TOLEO MAALUM Na. 231 | Wizara ya Madini | Mei 2019

# JARIDA LA NCHI YETU
TANZANIA

## MABADILIKO & UKUAJI

MADINI YETU,UCHUMI WETU, TUYALINDE.







Rais Magufuli Aipa Hadhi Sekta ya Madini ... Uk 3

Geita Lulu ya Madini Tanzania ... Uk 36



# Karibu Wizara ya Madini

## DODOMA

**Wizara ya Madini,**
**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**S.L.P 422,**
**40474 Dodoma.**

**Simu:** +255 26230051,
**Nukushi:** +255 26 2322282
**Baruapepe:** ps@madini.go.tz

**TOVUTI**
www.madini.go.tz

Madini Tanzania | Wizara ya Madini | Wizara ya Madini



# BODI YA WAHARIRI



**Mwenyekiti:**
Prof. Simon Msanjila
Katibu Mkuu
Wizara ya Madini

**Mhariri Kiongozi:**
Dkt. Hassan Abbasi
Mkurugenzi - Idara ya Habari - Maelezo

**Wajumbe:**
Rodney Thadeus
Terence Ngole
Dkt. Godfrey Nyamrunda
Asteria Muhozya
Elias Malima

**Wasanifu Jarida:**
Abubakari W. Kafumba
Kelvin N. Kanje


JARIDA LA NCHI YETU
LIMEANDALIWA KWA USHIRIKIANO WA
WIZARA YA MADINI NA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
(IDARA YA HABARI - **MAELEZO**)

# WIZARA YA MADINI




Wizara ya Madini,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 422,
40474 Dodoma.
Simu: +255 26230051,
Nukushi: +255 26 2322282
Baruapepe: ps@madini.go.tz
Tovuti: www.madini.go.tz

SALAMU ZA PONGEZI



**Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# Pongezi Maalum kwa Rais

MEI 2019


Uongozi wa Wizara ya Madini unampongeza kwa dhati Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Serikali anayoiongoza, ambapo katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake ameimarisha na kusisitizia usimamizi wa rasilimali za Taifa hususani madini ili kunufaisha Taifa kwa ujumla.

Katika kipindi cha uongozi wake, Wizara imefanikiwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Madini, Miongozo na Kanuni za Sekta ya Madini ili kuhakikisha rasilimali hii inawanufaisha Watanzania na kuongeza mapato ya Serikali na kuongeza ukusanyaji wa maduhuli na hii imeonesha wazi nia ya Wizara ya Madini kutekeleza kwa vitendo maono ya Mhe. Rais kuwa "Rasilimali ya Madini Iwanufaishe Watanzania."

Tunawiwa kwa namna ulivyosaidia sisi kufika hapa. Hatuna cha kukulipa isipokuwa kukuahidi kazi zaidi na uadilifu zaidi. Na kwa sababu hiyo basi, tunalitoa toleo hili maalum kuwa ni shukrani kwako na tunakuombea afya njema na nguvu zaidi katika kuendelea kuliongoza Taifa letu.

1 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 7 Oktoba, 2017 alifanya marekebisho ya Hati ya majukumu ya Waziri (Kipengele cha 144 tarehe 22 Aprili, 2016) Katika marekebisho hayo, Rais ameunda Wizara ya Madini ambayo ina mamlaka ya kuunda na kufuatilia utekelezaji wa Sera za Madini; Migodi, Utafiti wa Kijiografia; Shughuli za Tume ya Madini; Kuongeza thamani katika Viwanda vya Madini; Ushirikishwaji wa Wazawa wa Tanzania; Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo wa Madini; Maendeleo ya Kiutendaji na Maendeleo ya Rasilimali watu, Idara za ziada za Wizara, Mashirika ya Kiserikali, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara hii.

# SALAMU KUTOKA KWA WAZIRI WA MADINI
# SEKTA YA MADINI IMEANZA KUWA BARAKA



Kwa niaba ya Wizara ya Madini, napenda kuwakaribisha wapendwa wasomaji wetu na wadau wa Sekta ya Madini nchini katika Toleo hili Maalum la Jarida la NCHI YETU Tanzania ambalo limesheheni yale ambayo tumeyasimamia katika miaka hii mitatu.

Tumekamilisha utoaji wa jarida hili katika kipindi muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu; Serikali ya Awamu ya Tano ilishatimiza Miaka Mitatu sasa inaelekea minne lakini pia tupo katika kipindi muhimu cha utekelezaji wa kimageuzi wa sekta mbalimbali ikiwemo madini.

Katika kipindi hiki Tanzania na Dunia kwa ujumla wake imeshuhudia mabadiliko makubwa katika uendeshaji sekta nzima ya madini; Muundo wa Wizara, taasisi za kusimamia sekta ya madini, kutungwa kwa sheria mpya zinazosaidia kuwa na usimamizi bora wa madini yetu lakini pia tumeongeza kasi ya ushirikishaji wadau wa sekta hii.


Mabadiliko haya yanalenga kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kuhakikisha kuwa rasilimali madini inageuka kutoka "laana" iliyosababisha machafuko na umaskini kwingineko duniani hadi kuwa baraka na chachu ya ujenzi wa Tanzania bora ijayo.

Ni kwa sababu hii basi nikiwa Msimamizi Mkuu wa utekelezaji wa sera, sheria na ufanisi wa kitaasisi katika kufikia azma hiyo ya Mheshimiwa Rais, nikiri tu kuwa pamoja na changamoto za kikazi, kila uchao mimi na watendaji wangu wakuu tunafarijika kuona mafanikio yaliyokwishaanza kupatikana na namna mafanikio hayo yanavyochagiza maendeleo ya Taifa.

Nitumie fursa hii kumpongeza na kumshukuru Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na wasaidizi wake wakuu; Makamu wa Rais. Mhe. Mama Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa nia yao thabiti na miongozo yao kwetu kila mara wanapoona kuna jambo la kutufikishia.

Nawashukuru pia Mawaziri watangulizi wangu katika Wizara hii kwa kuweka misingi thabiti, Watendaji wa Wizara na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila, Wakuu wa Mikoa kote nchini ambao raslimali zetu za madini zipo katika mikoa yao kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa, watendaji wengine wa taasisi za umma na wadau wote wa sekta binafsi.

Narudia tena, kwa viongozi wetu na wadau wote wa madini, hatutawaangusha na tutasimamia falsafa na kaulimbiu yetu kwamba: "Madini Yetu, Uchumi Wetu, Tuyalinde."



**MHE.DOTO MASHAKA BITEKO (Mb)**
WAZIRI WA MADINI

# SALAMU KUTOKA KWA KATIBU MKUU



**TUTAENDELEA KUSIMAMIA UKUAJI SEKTA YA MADINI**

Ninayo furaha kuwakaribisha wasomaji wetu wote kusoma toleo hili maalum la sekta ya madini katika jarida hili kongwe la NCHI YETU Tanzania, linalochapishwa na Serikali kupitia Idara ya Habari - MAELEZO.

Kutolewa kwa chapisho hili maalum, kama alivyowasilisha Mhe. Doto Biteko, Waziri wa Madini, kunakuja wakati muhimu sana katika sekta ya madini nchini kutokana na mageuzi yanayoendelea chini ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Baadhi ya mageuzi hayo ni:

Katika mwaka wa fedha 2017-2018 sekta ya madini iliongoza kwa ukuaji nchini kwa kukuwa kwa takribani asilimia 18, ikilinganisha na mwaka wa fedha wa 2016-2017 ambapo sekta ilikua kwa asilimia 12. Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 makusanyo ya maduhuli yalikuwa TZS 210,185,986,188.33 na kuongezeka mwaka 2016/2017 kufikia TZS 214,506,024,960.99.

Mwaka 2017/18, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 194,633,498,763 lakini ikavuka lengo kwa kukusanya TZS bilioni 301.6 sawa na 155% ya malengo. Katika mwaka 2018/2019 maduhuli yameendelea kukua ambapo mpaka Februari 2019 pekee, tayari Jumla ya TZS 218,450,606,093 zilikusanywa, sawa na asilimia 106 ya lengo la kipindi hicho.

Kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli kumewezesha sekta ya madini kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 4.8 kwa kipindi cha Miaka ya Fedha 2016/2017 na 2017/2018.

Aidha, baada ya Serikali kukamilisha ujenzi wa ukuta kuzunguka machimbo ya Tanzanite, Mirerani, na kuweka miundombinu mingine wezeshi kama vile Jumba la Wafanyabiashara wa Madini (Brokers House), Kituo cha Pamoja cha Huduma za Biashara ya Madini (One Stop Centre) na uwekaji wa miundombinu ya umeme na mifumo ya kidijitali ya ulinzi (CCTV security systems), uzalishaji umeongezeka. Utoroshaji wa madini umepungua na kuongeza uzalishaji wa Tanzanite kutoka Kg. 147 (mwaka 2017) hadi Kg. 781 (mwaka 2018).

Serikali pia imetumia TZS Bilioni 11.9 kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kujenga vituo saba vya umahiri (centers of excellence), vituo vitatu wa mfano (demonstration centres), mafunzo kwa wachimbaji wadogo na ununuzi wa mashine ya uchorongani.

Natumia fursa hii kuahidi kuwa mafanikio haya ni matokeo ya watendaji wote katika sekta ya madini kutimiza wajibu wao na kwa niaba yao niahidi kuwa tutaendelea kufanyakazi zetu kwa ubunifu, kujituma, kujitoa ili kuhakikisha mchango wa sekta yetu unazidi kukua.

Nawatakia usomaji mwema wa jarida hili ili kufahamu zaidi Sekta ya Madini.

**PROF. SIMON SAMWEL MSANJILA**
KATIBU MKUU
WIZARA YA MADINI

# Tahariri

## SEKTA YA MADINI; TUMETHUBUTU, TUMEWEZA

Sekta ya Madini imeonesha tukithubutu, tunaweza. Miaka mitatu iliyopita sekta aushi ya madini lilikuwa eneo la lawama, minong'ono kuwa tunaibiwa na wasiwasi mkubwa kuwa kama nchi nyingine, Tanzania nayo inaelekea katika kile kinachojulikana kama "laana ya rasilimali" kutokana na kutokuwepo kwa mwelekeo thabiti wa sekta hiyo kuinufaisha nchi na wananchi wake.

Leo ikiwa ni miaka mitatu baadaye, Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imechukua hatua; haikukubali kuona suala hili linaendelea kwa staili ya watanzania kuendelea kulalamika.

Makala zilizomo katika toleo hili maalum zinashadidisha uhalisia wa mageuzi makubwa ambayo Serikali ya awamu ya Tano imeyatekeleza katika kuhakikisha sekta hii inaondoka kutoka kuwa ya lawama hadi kuwa ya maana kwa maslahi ya Tanzania na wananchi wake.

Mageuzi yaliyogusa mifumo ya kisheria, kitaasisi, uongezaji thamani na kuchagiza ufanisi katika kuhakikisha kuwa sekta ya madini inalinufaisha Taifa letu, kwa hakika yameanza kulipa na ni imani yangu, kama anavyokiri Mhe. Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini, katika utangulizi wake katika jarida hili, ni wazi kuwa mabadiliko katika ongeze-ko la uzalishaji, mapato kwa Taifa na kipato kwa wachimbaji, ni faraja kuu inayopaswa kuwatia moyo wote walioko katika mnyororo wa kuisimamia sekta hii waendelee kuongeza kasi.


Nimpongeze Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wote kwa maono, maonyo, na zaidi moyo na kujitoa kwao kuhakikisha sekta hii inakuwa ya kipaumbele katika kuwakomboa Watanzania. Hongera Rais, Hongera Wizara ya Madini na Hongera kwa wote walioshiriki katika safari hii ya mageuzi.

Kwa niaba ya wenzangu katika jukumu hili adhimu la kikatiba na kisheria la kuwahabarisha wananchi, naahidi kwamba, nasi tutatumia kila aina ya nyenzo, akili na Maarifa kushiriki kwa kuyatangaza na kuyatetea mazuri yanay-oendelea kujitokeza katika sekta hii na nyingine za Taifa. Aidha, tunazikaribisha Wizara na taasisi mbalimbali za umma kuiga mfano huu wa sekta ya madini kwa kuungana nasi katika kutangaza mafanikio yaliyopa-tikana.


Kwa makala na picha zilizosheheni humu kueleza mafanikio yaliyopatikana, kama Taifa, uthubutu wetu umedhihiri-sha kuwa tunaweza na hakika "Madini Yetu, Uchumi Wetu, Tuyalinde."

**Dkt. Hassan Abbasi - Mhariri**
Mkurugenzi - Idara ya Habari - MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali.

# Viongozi wa Wizara ya Madini na Taasisi Zake




WAZIRI WA MADINI,
**Mhe. DOTO BITEKO (Mb)**




NAIBU WAZIRI WA MADINI,
**Mhe. STANSLAUS NYONGO (Mb)**



KATIBU MKUU WIZARA YA MADINI,
**Prof. SIMON MSANJILA**




KAMISHNA WA MADINI,
**MHANDISI DAVID MULABWA**




KATIBU MTENDAJI WA TUME YA MADINI
**Prof. SHUKRANI MANYA**




KAIMU MTENDAJI MKUU WA TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST)
**YORKBERTH MYUMBILWA**



KAIMU MTENDAJI MKUU WA SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)
**KANALI SYLVESTER GHULIKU**



KAIMU MRATIBU WA KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA
**ERICK MPESA**



KAIMU KATIBU MTENDAJI WA TAASISI YA UHAMASISHAJI, UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI ZA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA (TEITI, )
**MARIAM MGAYA**




KAIMU MKUU WA CHUO CHA MADINI DODOMA (MRI)
**FREDRICK MANGASINI**

# YALIYOMO

















PMI








107
033
261









# YALIYOMO
## KATIKA JARIDA HILI

### UTANGULIZI


**i. Pongezi Maalum kwa Rais**

**ii. Salamu Kutoka kwa Waziri wa Madini**

**iii. Salamu Kutoka kwa Katibu Mkuu**

**iv. Tahariri**

**v. Viongozi wa Wizara na Taasisi zake**




### MAKALA SEKTA YA MADINI


3 Rais Magufuli Aipa Hadhi Sekta ya Madini

8 Ijue Wizara ya Madini

12 Kuyaongezea Madini Thamani, Mwarobaini wa Mapato Zaidi

16 Ukuta wa Mirerani Waongeza Mapato

21 Wachimbaji Wadogo Tumeinuliwa, Asante Mhe. Rais Magufuli

27 Ushirikishwaji wa Wazawa. Mfumo Mpya wa Kuchangia Jamii Kuziinua Halmashauri

30 Zijue Faida za Sheria mpya Zinazosimamia Sekta ya Madini

36 Geita Mji wa Dhahabu

40 Jicho la Wanahabari katika Mabadiliko Sekta ya Madini Tanzania

42 Dunia ilivyofuatilia Mageuzi ya JPM Sekta ya Madini


### MAKALA TAASISI ZA WIZARA


46 Tume ya Madini Yavuka Lengo Ukusanyaji wa Maduhuli

48 GST Yakamilisha Tafiti Kuwainua Wachimbaji Madini


52 STAMICO Yaongeza Ufanisi Kusaidia Sekta ya Madini

54 Chuo cha Madini Chachu ya Kuiongezea Sekta Thamani

57 TEITI Yaimarisha Uwazi, Uwajibikaji Sekta ya Madini

62 TGC Chachu kufikia Lengo kuyaongezea Thamani Madini



### MAKALA ZA MIGODI


66 MGODI WA BUSOLWA: Tunanufaika na Mageuzi ya JPM

69 Udhibiti Sekta ya Madini waongeza Uzalishaji MWADUI



1

# MAENDELEO & UKUAJI

## MAENDELEO KATIKA SEKTA YA MADINI NDANI YA KIPINDI CHA MIAKA MITATU CHINI YA UONGOZI WA RAIS WA AWAMU YA TANO MHE. DKT. JOHN POMBE MAGUFULI



2



# NI MAGEUZI YA KIHISTORIA

## RAIS MAGUFULI AIPA HADHI SEKTA YA MADINI

- Mapato Yaongezeka Kutoka Lengo la Shilingi **Bilioni 194**
- Makusanyo Halisi ya Shilingi **Bilioni 301 Mwaka 2017/18**



Na **Asteria Muhozya**
Wizara ya Madini

Ni Miaka Mitatu ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kuhuisha safari ya mageuzi katika sekta mbalimbali nchini Tanzania. Kwa Sekta ya Madini ilikuwa ni miaka mitatu ya kuanzisha na sasa Watanzania kuanza kuiona thamani halisi ya sekta hii muhimu kwa Taifa na kwa mwananchi mmoja mmoja.

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu, Rais Magufuli na Serikali yake kwa ujumla ametoka kwenye kutoa ahadi kwa wananchi mwaka 2015 kuwa atahakikisha sekta ya madini inakuwa na tija katika uchumi na maendeleo ya Watanzania hadi kutekeleza ahadi hiyo kivitendo kwa kutekeleza mambo 6 yafuatayo ya kimageuzi:

## 1. Mabadiliko ya Kitaasisi

Katika kutekeleza azma yake ya kuifanya sekta ya madini isimame na kuwa na mchango kwa Taifa, Rais Magufuli amefanya mabadiliko kadhaa ya kitaasisi katika miaka yake mitatu ikiwemo kuunda Wizara ya Madini inayojitegemea na yenye dhamana ya moja kwa moja katika sekta hii.

Licha ya mabadiliko hayo, kufuatia mabadiliko Sheria za Madini ya Mwaka 2017, taasisi na baadhi ya majukumu yaliyokuwa Wizarani katika kusimamia sekta ya madini viliunganishwa na kuundwa Tume ya Madini.

Tume hii imeleta mageuzi makubwa katika usimamizi wa sekta ya madini kuanzia kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa leseni hizo, kusimamia mapato ya Serikali katika madini na kwa ujumla kuhakikisha madini yanalinufaisha Taifa kwanza-Makala mahsusi kuhusu kazi za Tume itaelezea zaidi mafanikio yao.

## 2. Sheria Mpya za Madini

Mbali na mageuzi ya kitaasisi, Serikali ya Awamu ya Tano pia imeweka historia kwa kutunga sheria mpya mbili zenye lengo la kuhakikisha kuwa madini yetu yanalinufaisha Taifa letu na kuwa chachu ya maendeleo ya Tanzania.

Mosi, ni Sheria ya Mamlaka Ya Nchi (Kuhusu Umiliki wa Madini) Na. 5, 2017 ambayo inatamka bayana kuwa raslimali za madini ni mali ya Watanzania ikisimamiwa kwa niaba yao na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Vifungu vingine muhimu na mageuzi mengine yaliyoletwa na Sheria hii yanaanishwa kwa kina katika makala ilioyoandikwa mahsusi kuzichambua sheriampya.

Pili, ni Sheria ya Mamalaka ya Mamlaka ya Mapitio (Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi Katika Mikataba ya Maliasili za Nchi) Na. 6, 2017. Sheria hii inaipa Serikali ya Tanzania fursa ya kujadiliana na kuondoa vifungu visivyo na maslahi kwa nchi katika mikataba ya madini nchini.

Mafanikio ya Sheria hii yameshaanza kuonekana ambapo Serikali imeanza majadiliano na makapuni kadhaa makubwa ya madini nchini ikiwemo Acacia na TanzaniteOne. Tayari makubaliano kadhaa kati ya Serikali na kampuni hizi yameshafikiwa ikiwemo kuongeza hisa za Serikali na Serikali kupata mapato zaidi. Mageuzi mengine yaliyoletwa na Sheria hii yanaanishwa kwa kina katika makala iliyoandikwa mahsusi kuzichambua sheria mpya na kuchapisha katika kurasa zijazo za toleo hili.

Tatu, ni mabadiliko kwenye Sheria ya Madini ya 2010 yaliyofanyika kupitia Mabadiliko ya Sheria yaani the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017. Mabadiliko haya yaliyoanza kutumika kuanzia 7/7/2017, yamefanya mabadiliko kadhaa katika Sheria ya Mwaka 2010 ikiwemo:

- **Kuanzishwa kwa Tume ya Madini (The Mining Commission);**
- **Kufutwa kwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini (Tanzania Mineral Audit Agency - TMAA).**



## 3. Mkutano wa kihistoria wa Rais na wachimbaji wadogo

Mbali ya mifumo ya kitaasisi na kishe-ria, kama kuna mageuzi mengine makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ni utayari wa Serikali katika kukutana, kujadiliana na kuzielewa changamoto za kisekta ili kuzitafutia ufumbuzi.

Katika hili, sekta ya madini haitalisahau tukio la Januari 22, 2019 baada ya wadau wa sekta hiyo kukutana ana kwa ana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Pombe Magu-fuli na kujadili kwa pamoja fursa na changamoto zilizopo katika sekta hiyo na namna ya kuzitatua.


Katika mkutano huo ambao pia ulihud-huriwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais Magufuli hakuso-ma hotuba kama ilivyozoeleka, bali alitumia takribani saa saba kusikiliza kero, chanamoto na maoni kutoka kwa wachimbaji wadogo, wa kati, wakubwa na wafanyabiashara wa madini nchini.

Wachimbaji na wafanyabiashara ya madini walieleza mambo mengi lakini kubwa ikiwa ni kero kuhusu tozo na kodi mbalimbali zinazotozwa kwa wachimbaji na wafanyabiashara ya madini, kukosekana masoko maalumu ya kuuzia madini na bei elekezi za madini jambo ambalo wadau waliona ni kikwazo ambacho kinachochea utoroshaji wa madini nje ya nchi.Kwa upande wake, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini Tanzania (FEMATA) Bw.John Bina, alimhakikishia Mhe. Rais Magufuli kuwa endapo wachimbaji wadogo ambao idadi yao ni karibu milioni sita wataondolewa kero za kutozwa kodi nyingi na kuwekewa mazingira bora ya biashara ya madini ikiwemo uwepo wa masoko maalum ya kuuza madini, watachangia zaidi tofauti na ilivyo sasa.

## 4. Maagizo ya Rais

Baada ya kusikiliza kero hizo, Mhe. Rais aliiagiza Wizara ya Madini na Wizara ya Fedha kuharakisha kero zilizoelezwa na wadau zinatatuliwa kwa haraka ili mchango wa sekta hiyo kwa uchumi wa nchi uongezeke.

Baadhi ya kero zilizotajwa kutakiwa kufanyiwa utatuzi wa haraka ni utitiri wa kodi na tozo katika biashara ya madini, kuzuia utoroshaji wa madini nje ya nchi na masoko ya uhakika kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini.





Madini ya Dhahabu

### 5. Wizara Zatekeleza Maagizo

Siku nne tu baada ya agizo la Rais Magufuli alilolitoa Januari 22, 2019, Wizara ya Madini kwa kuishirikiana na taasisi nyingine za Serikali na kuweka mkakati wa kutatua kero mbalimbali. Baadhi ya kero ambazo mpaka sasa zimeshatatuliwa ni:

- Kuondoa asilimia 18 ambayo ni Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) waliyokuwa wakitozwa wafanyabiashara wadogo wa madini wanapouza madini yao;

- Kuondoa Kodi ya Zuio (Witholding Tax) ya Asilimia 5 iliyokuwa ikitozwa kwa kwa wachimbaji wadogo wa madini wanapouza madini yao;

- Kufunguliwa Soko la Kwanza Nchini na la Tatu Afrika la Madini ambalo lilifunguliwa Machi 17, 2019 mkoani Geita na Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Masoko mengine mengi yakafuata kufunguliwa.

Mafanikio haya yanamgusa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na anawaeleza Watanzania kupitia mkutano wake Geita siku anazindua soko la madini aliposema:

"Naishukuru Wizara ya Madini, Mkoa wa Geita na Tume ya Madini kwa kusimamia na kutekeleza maagizo ya Serikali kwa wakati. Naviagiza vyombo vya Ulinzi na Usalama vihakikishe soko hili linapata ulinzi wa kutosha muda wote ili watendaji, mali zitakazokuwemo, vitendea kazi na miundombinu yote iwe salama muda wote." Naye Waziri wa Madini, Dotto Biteko anaahidi Wizara yake kuendelea kusimamia kikamilifu mageuzi katika sekta ya madini akiwataka wadau wote nchini kutoa ushirikiano.

### 6. Mageuzi Yawagusa Wadau

Kutokana na mageuzi makubwa ikiwa ni matokeo ya mkutano wa Rais na wadau wa sekta ya madini na hatua mbalimbali zilizochukuliwa, wadau wanaojishughulisha na madini ya tanzanite waliishukuru Serikali kwa kufanya maandamano ya amani Februari 16, 2019 ikiwa ni namna ya kumpongeza Rais Magufuli na watendaji wake

Akizungumza katika maandamano hayo, Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Mkoa wa Manyara (MAREMA),

Justin Nyari alieleza jinsi walivyofurahishwa baada ya Serikali kuondoa baadhi ya kodi kwa wachimbaji na kutolewa mwongozo wa uongezaji thamani. Tayari mageuzi mbalimbali yameonesha mafanikio katika Taifa kuelekea kupata mapato yake stahiki. Kwa ujumla mapato ya madini yameongezeka na kuipa Serikali uwezo wa kugharamia huduma nyingine.

Katika mwaka 2017/18 lengo la kukusanya TZS Bilioni 194 lilivukwa kwa zaidi ya mara mbili ambapo mapato kutoka sekta nzima ya madini yaliongezeka hadi kufikia TZS Bilioni 301. Hatua za Serikali ikiwemo usimamizi vinatarajiwa kuongeza zaidi mchango wa sekta hii.



Niliagiza yaanzishwe masoko ya Madini lakini nashangaa kama Mkuu wa Mkoa wa Geita ametekeleza wengine mnasubiri nini?. Wewe wa Mbeya nakupa siku 7 hapa Chunya soko lianze. Na hii ni kwa wengine pia.



# #JPM MBEYA

# MEI, 2019

@maelezoTV

Msemajimkuuwaserikali

# IJUE WIZARA YA MADINI




*Jengo la Wizara ya Madini lililopo katika Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma*

H Historia ya uchimbaji wa madini hapa chini inaanzia miaka ya 1890 wakati wafanyabiashara kutoka bara la Asia hususani nchi za Kiarabu walipofika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na kuanza biashara ya madini hasa ya dhahabu, shaba, fedha, chuma na chumvi.

Kati ya miaka ya 1920 na 1930 shughuli za uchimbaji madini zilizidi kushamiri nchini hasa baada ya soko na bei ya madini ya metali na vito kuongezeka duniani.

Kutokana na msukumo huo mkubwa kutoka soko la Dunia, Mgodi mkubwa wa Almasi wa Williamson Diamond Limited ulifunguliwa miaka ya 1940 katika eneo la Mwadui mkoani Shinyanga.

Baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961, uendshaji wa sekta ya madini uliwekwa chini ya Serikali huku Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) likisimamia shughuli hizo na baadae Mgodi huo ulikuwa moja ya migodi mikubwa sana duniani na uliifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye shughuli kubwa za uchimbaji madini kuwa chini ya Shirika la Uchimbaji Madini la Taifa (STAMICO) baada ya shirika hilo kuanzishwa mwaka 1972 na kupewa jukumu kuu la kuisimamia shughuli zote za madini nchini.

Utaratibu huo wa usimamizi uliendelea hadi miaka 1990 ambapo nchi yetu ilifanya marekebisho makubwa katika sera za kiuchumi ili kuvutia uwekezaji, hasa kutoka nje ya nchi.Kutokana na mabadiliko hayo, migodi mikubwa na ya kati ilianzishwa nchini, na mchango wa sekta ya madini ukaongezeka.

Hata hivyo, baada ya miaka kadhaa, mchango wa sekta ya madini ulionekana kutokuwa mkubwa sana kutokana na changamoto kadhaa ikiwemo utoroshwaji wa madini, ukwepaji kodi, na umiliki na ushiriki mdogo wa Watanzania katika miradi ya madini.

Kutokana na mabadiliko hayo, migodi mikubwa na ya kati ilianzishwa nchini, na mchango wa sekta ya madini ukaongezeka.

Hata hivyo, baada ya miaka kadhaa, mchango wa sekta ya madini ulionekana kutokuwa mkubwa sana kutokana na changamoto kadhaa ikiwemo utoroshwaji wa madini,ukwepaji kodi, na umiliki na ushiriki mdogo wa Watanzania katika miradi ya Madini.

Kutokana na changamoto hizo, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli iliamua kuifanyia marekebisho Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ambapo pamoja na mambo mengine, iliundwa Wizara ya Madini baada ya kuivunja iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini kupiti.Hati ya Majukumu (Instrument) Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 na Marekebisho yake ya Oktoba 7, 2017.

Kutokana na mbadiliko hayo makubwa ya Sheria ya mwaka 2017, majukumu mapya ya Wizara ya Madini ni pamoja na;

- **Kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mikakakti na mipango ya kuendeleza sekta ya madini.**
- **Kusimamia migodi na kuhamasisha shughuli za chimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa kutumia tafiti za kijiofizikia na kijiolojia (geophisical na geological surveys).**
- **Kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini.**
- **Kukuza ushiriki wa wazawa (local content) kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini.**
- **Kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo.**
- **Kusimamia Taasisi na mamlaka zilizoko chini ya Wizara.**

Ili kurahisisha utelekezaji wa majukumu hayo Wizara ya Madini inaundwa na Idara Kuu tatu, ambazo ni Idara ya Madini, Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, na Idara ya Sera na Mipango.

Idara ya Madini inasimamiwa na Kamishna wa Madini ambaye jukumu lake kuu ni kumshauri Mhe. Waziri wa Madini kuhusu masuala yote yanayohusu madini.

Ili kutekeleza majukumu yake vizuri na kwa ufanisi, Kamishna wa madini anasaiwa na vitengo vitano ambavyo ni Kitengo cha Uendelezaji Migodi, Kitengo cha Ushirikishwaji watanzania, Kitengo cha Uongezaji Thamani na Kitengo cha Wachimbaji Wadogo na Mazingira.

Vitengo hivyo vinasimamiwa na Makamishna wasaidizi.

Vilevile, Wizara ina jumla ya Taasisi sita ambazo ni Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Chuo cha Madini (MRI); Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi katika Rasilimali za Madini Mafuta na Gesi Asilia (TEITI).


Kutokana na majukumu na muundo huo mpya, Wizara ya Madini imejiwekea malengo kadhaa ikiwepo kuhakikisha mchango wa sekta kwenye pato na uchumi wa Taifa unaongezeka maradufu kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2025 kutoka asilimia 4.8 ya sasa, Kuboresha usimamizina uendelezaji wa rasilimali madini, kuboresha mazingira ya uchimbaji mdogo na kuimarisha usimamizi wa mazingira katika sekta ya madini.



***Mhe. Doto Mashaka Biteko,*** *Waziri wa Madini.*



# THAMANI YA MADINI





# Kuyaongezea Madini Thamani, Mwarobaini wa Mapato Zaidi

Na **Mwandishi Wetu**
Wizara ya Madini

Mara kadhaa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, amekuwa akisisitiza kuwa njia pekee kwa Tanzania kunufaika na sekta ya madini ni kuyaongezea thamani ili yapate bei nzuri katika masoko ya kimataifa kupitia viwanda vya uongezaji thamani ambavyo pia vitatoa ajira kwa watanzania.

Ili kutekeleza hilo, kupitia Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, pamoja na marekebisho ya mwaka 2017, Wizara ya Madini imeendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini kwa lengo la kuongeza mnyororo wa thamani ili kuleta tija kwa wachimbaji na Serikali kwa ujumla.

Miongoni mwa mikakati ya kuongeza myororo wa thamani ya madini ni pamoja na kutoa mafunzo ya usonara, ukataji wa madini, uchongaji wa madini pamoja na elimu ya jimolojia (sayansi ya kuyatambua madini na kupima thamani yake).

Aidha, hatua nyingine ni kwa Serikali kuweka zuio kisheria la kusafirisha madini ghafi pamoja na makinikia (concentrates) nje ya nchi ili kuhakikisha kuwa madini yanayochimbwa hapa nchini yanaongezewa thamani kabla ya kusafirishwa.

Kufanyika kwa shughuli na juhudi hizi za kisera, kisheria na kimafunzo katika uongezaji thamani madini hapa nchini kunatoa fursa ya ajira, kuongeza mapato, kuimarisha usimamizi wa madini na kuhawilisha teknolojia (technology transfer) na hivyo kuleta manufaa zaidi kwa Taifa.

Katika kuhakikisha agizo la Rais Dkt. John Pombe Magufuli la kuzuia usafirishaji wa madini ghafi nje ya nchi,ikiwa ni jitihada za kuyaongezea thamani hapa nchini, Wizara ya Madini imeandaa Muongozo wa Uongezaji Thamani Madini wa Mwaka 2019, unaoainisha kiwango cha kila madini kinachotakiwa kufikiwa kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi.



Pia muongozo huo umeruhusu baadhi ya madini ghafi hususani madini ya vito kusafirishwa nje ya nchi kwa kuwa yanahitaji teknolojia ya juu kuyaongezea thamani hadi hapo Tanzania itakapokuwa na uwezo huo.

Aidha, muongozo huo umeweka masharti ya kusafirisha madini ghafi ya viwandani kwa kupata kibali maalum kutoka Tume ya Madini ambayo itajiridhisha kwanza juu ya uhitaji wa madini hayo kutumika yakiwa ghafi na kuona kama hakuna athari katika viwanda vya ndani.

Faida nyingine, mbali na ajira na kuongeza mapato ya nchi, kuongeza myororo wa thamani katika madini kutaisaidia nchi kufikia azma yake ya kuzuia utoroshaji wa madini yaliyokuwa yanatoroshwa kwenda nje ya nchi kwa kisingizio cha kukosa utaalamu wa kuyaongezea thamani hapa nchini.

Hatua nyingine za kujenga mazingira wezeshi hapa nchini, na katika kuhakikisha madini yaliyoongezewa thamani haya nchini yanapata masoko, Wizara ya Madini imeandaa Kanuni za Masoko ya Madini za mwaka 2019, ambazo zimetoa mwongozo wa uanzishwaji na uendeshaji wa masoko ya madini nchini.

Uwepo wa masoko hayo ya madini, utarahisisha shughuli za biashara ya madini kwa kuwapeleka wanunuzi karibu na wazalishaji madini hivyo kuimarisha udhibiti wa utoroshaji madini nje ya nchi, pamoja na kuwa na takwimu sahihi za uzalishaji hususani kutoka kwa wachimbaji wadogo na kuipatia Serikali mapato stahiki.

Wizara ya Madini pia imeandaa Waraka wa Sheria ya Uongezaji Thamani Madini, ili kuwezesha shughuli za Uongezaji Thamani Madini kama usonara, usanifu uchongaji, ung'arishaji na ufinyanzi kusimamiwa kikamilifu kisheria.

Kukosekana kwa Sheria inayosimamia shughuli za uongezaji thamani, kumesababisha kiasi kikubwa cha madini ya dhahabu, fedha na vito kinachozalishwa na wachimbaji wadogo kutofahamika.

Pia kutokuwepo kwa sheria hiyo kunasababisha kutokuwepo kwa takwimu sahihi za shughuli za uongezaji thamani ya madini kama vile kiwango na thamani ya madini kinachotumika katika shughuli za usonara.

Sheria hiyo pia itaondoa ama kudhibiti mwanya wa kutorosha madini yaliyoongezewa thamani, kupitia bidhaa za usonara kama mikufu ya dhahabu, pete na vidani. Eneo hili hutumika sana katika utoiroshaji wa madini.

Sanjari na hatua hizo, Serikali kupitia Wizara ya Madini imeweka pia zuio la uingizaji wa makaa ya mawe na jasi kutoka nje ya nchi na kuwataka wenye viwanda vya saruji na watumiaji wengine wa madini hayo hapa nchini kununua kutoka kwa wachimbaji wa hapa nchini.

Wanunuzi pia wametakiwa kuwa na mikataba na wachimbaji ili kuwapa uhakika wa soko na kuwawezesha kutumia mikataba hiyo kuombe mikopo kutoka kwenye benki mbalimbali ili kuboresha uchimbaji wao.

Vilevile, serikali inaendelea kuhakikisha kwamba, wachimbaji wa madini ya viwandani kama kaolin, quartz, clay,feldspar magnetite, limestone, dolomite, gypsum, bauxite, pozzolana na red soil wanauza madini hayo kwenye viwanda vya saruji, vigae na chupa, kwa bei ambazo zitapelekea uchimbaji kuwa endelevu pamoja na viwanda hivyo kuwa na uhakika wa malighafi.

Aidha kwa sasa, hatua nyingine muhimu ni waombaji wa leseni za biashara za madini ya vito, hutakiwa kuwa na mashine za kukata na kung'arisha madini walizo nazo hapa nchini.

Kwa upande wa leseni zinazomilikwa na Watanzania wanatakiwa kuwa na mashine zisizopungua tano na kwa leseni zenye ubia na wageni wanatakiwa kuwa na mashine zisizopungua 30.

Masharti hayo ya kisheria yamesaidia kuwepo kwa viwanda vya ukataji madini ya vito hapa nchini. Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu shughuli za uongezaji thamani madini ya vito ili kufikia viwango walivyofikiwa na nchi kama India na Thailand.

*Mwanafunzi akipata mafunzo kivitendo ya ukataji na ung'arishaji madini ya vito katika Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)*





# UKUTA WA MIRERANI WAONGEZA MAPATO

## UZALISHAJI WA TANZANITE





Na **Mwandishi wetu**
**Wizara ya Madini**

UAMUZI wa kujenga ukuta katika eneo la wachimbaji wadogo na kati wa Tanzanite eneo la Mirerani, Wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara, umeendelea kuzaa matunda baada ya uzalishaji na mapato kuongezeka.

Ukuta huo ulianza kujengwa mwaka 2017 kufuatia Rais Dkt. John Pombe Magufuli kutoa agizo akilenga kudhibiti utoroshaji uliokithiri wa madini hayo.

Miezi kadhaa sasa baada ya ukuta huo kuzinduliwa mnamo mwaka 2018, mapato yameongezeka kufikia shilingi bilioni 1.436 mwaka 2018 ikilinganishwa na shilingi milioni 166.1 mwaka 2017 na shilingi milioni 71.7 kwa mwaka 2016 kutoka kwa wachimbaji wadogo na wa kati.

Lengo la ujenzi wa ukuta huo ambao wenyeji wa Mirerani wanauita "Ukuta wa Magufuli" ni kudhibiti wizi, upotevu wa mapato na utoroshwaji wa madini ya Tanzanite nje ya nchi.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Profesa Shukran Manya anasema kuongezeka kwa mapato kumechangiwa na kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa madini ya Tanzanite kutoka kwa wachimbaji wadogo na kati ambapo mwaka 2018 jumla ya kilo 781.204 zilizalishwa zikiwa na thamani ya shilingi bilioni 20.1 ambapo mrabaha ulikuwa shilingi bilioni 1.435 ikilinganishwa na kilo 147.7 mwaka 2017 na kilo 164.6 mwaka 2016 ambazo zote kwa pamoja zilikuwa na mrabaha wa shilingi milioni 337.8.

Ukuta huo umejengwa na kusimamiwa na wahandisi wa Ujenzi kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ikishirikisha Maafisa 34, Askari 287 na Vijana 2,038 wa Operesheni Kikwete na Opereshi Magufuli.

Ilichukua miezi mitatu tu ujenzi wa ukuta huo kukamilika na kuzinduliwa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli April 6, 2018 badala ya sita iliyopangwa awali na kugharimu shilingi bilioni tano.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa akiwemo Mgunduzi wa Madini hayo, Marehemu Jumanne Mhero Ngoma ambapo Serikali ilimtambua rasmi kama mgunduzi wa Tanzanite. Kihistoria madini ya Tanzanite yaligunduliwa mwaka 1967.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ukuta huo, Rais Dkt. Magufuli alisema Serikali imeujenga ukuta huo kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ili kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na Tanzanite, kudhibiti utoroshaji wa Tanzanite, kuongeza thamani ya Tanzanite na kuwafanya wafanyabiashara na wachimbaji wa madini hayo kufanyabiashara yao kwa uwazi zaidi.

Eneo hilo pia limewekewa kituo cha kuwakutanisha wanunuzi na wauzaji. "Hakuna kitakachoharibika, kampuni zote zitaingia mkataba na Serikali na watanunua hapa na watakaouza watayauzia hapa. Tutafungua mabenki na kuanzisha utalii wa madini," alisema Rais Magufuli... *Inaendelea Uk 18*

> ***Hakuna kitakachoharibika, kampuni zote zitaingia mkataba na Serikali na watanunua hapa na watakaouza watayauzia hapa. Tutafungua mabenki na kuanzisha utalii wa madini***
>
> Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli.**





# WADAU WA TANZANITE WAFURAHIA

Akisoma hotuba kwa niaba ya Chama katika moja ya vikao vya wafanyabashara wa madini na Wizara jijini Arusha, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini (TAMIDA), Sam Mollel anasema kuwa TAMIDA inaunga mkono juhudi zilizofanywa na Rais Dkt. Magufuli za ujenzi wa ukuta huo.

Alisema ujenzi huo umeleta udhibiti na umeongeza imani kubwa kwa wanunuzi wa madini hayo zikiwemo nchi za Marekani na Ulaya huku ukidhibiti ajira za watoto migodini na uingiaji holela katika machimbo hayo.

Naye mmoja wa wanunuzi wa Tanzanite, Lydia Mollel anaeleza manufaa aliyoyaona tangu ukuta ulipojengwa akisema:

"Baada ya ukuta kumekuwepo na usawa kati ya wanaume na wanawake kutokana na kwamba awali, wanaume matajiri waliweza kupata madini kwa muda wowote ambapo wao kama wanawake iliwalazimu kusubiri mpaka asubuhi."

Baada ya ujenzi zipo jitihada kadhaa zilizofanywa na wizara kufuatia maelekeo ya Mhe. Rais kuhakikisha Tanzanite inatambulika kimataifa kuhusu uhalisia wake, inadhibitiwa na inawanufaisha Watanzania.


Katika kuhakikisha hilo linaanza kutekelezwa, Serikali kupitia Wizara ya Madini tayari imeandaa Kanuni zifwatazo za "Mirerani Controlled Area" za mwaka 2018 ambazo zinatoa mwongozo wa namna shughuli za uchimbaji, biashara ya madini na huduma za jamii zitakavyoendeshwa ndani ya ukuta. Kanuni hizo zimesainiwa na Waziri wa Madini ,Mhe.Doto Biteko, tarehe 30 Januari, 2019.

Aidha, mbali ya ujenzi wa ukuta kuzunguka migodi, tayari Serikali inaendelea na ujenzi wa jengo maalum la Huduma za Pamoja ndani ya Ukuta (One stop Centre) ambapo shughuli zote za mauzo na minada ya madini zinafanyika.

Jengo hilo linajengwa na mkandarasi SUMAJKT kwa gharama ya shilingi bilioni 1,148,259,500. Aidha mifumo ya kamera za ulinzi imeshafungwa ili kuhakikisha usalama wa eneo husika.

Sambamba na hayo, tayari wizara imezindua jengo la biashara ya madini (brokers lounge) ndani ya ukuta, mahsusi kwa ajili ya uthaminishaji wa madini pindi yanapochimbwa migodini.

Aidha, kwa sasa Serikali inafanya jitihada za kupata Hati ya Utambulisho wa Kimataifa ya madini ya Tanzanite ambayo yanapatikana Tanzania pekee.




# UCHIMBAJI WA TANZANITE WAONGEZEKA KWA KIASI KIKUBWA

**TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA - GST**










TEMBELEA MAKUMBUSHO YA TAIFA YA JIOLOJIA YANAYOPATIKANA KATIKA TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST) , UTAJIFUNZA NA KUJIONEA MIAMBA NA MADINI MBALIMBALI YANAYOPATIKANA HAPA NCHINI TANZANIA.

## WASILIANA NASI:

**MTENDAJI MKUU,**

**TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA,**
**MTAA WA KIKUYU,**
**S.L.P 903,**
**DODOMA.**

+255 262 323020 | +255 262323020 | madini.do@gst.go.tz | http.gst.go.tz



# FEMATA

## WACHIMBAJI WADOGO TUMEINULIWA, ASANTE MHESHIMIWA RAIS MAGUFULI



Na **Asteria Muhozya**
Wizara ya Madini

Katika kutambua umuhimu wa Sekta ya Madini nchini, Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara ya Madini imejipanga kimkakati kuhakikisha inasimamia, inatekeleza na inasaidia ukuaji wa sekta hii hasa kwa kuwawezesha wachimbaji wadogo ambao kwa muda mrefu wamekuwa hawanufaiki na rasilimali hiyo.

Wizara pia imepata nguvu ya kutekeleza majukumu yake kutokana na dhamira ya dhati ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, ya kuhakikisha sekta ya madini inasimamiwa ipasavyo na inaleta tija kwa wachimbaji na Serikali kwa ujumla.

Akizungumza hivi karibuni na Jarida la Nchi Yetu, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini Tanzania (FEMATA), Bw. John Bina, anakiri kuwa nafasi ya wachimbaji wadogo kwa sasa ni kubwa katika kutoa mchango wao kwa Taifa.“Tunamshukuru sana Rais Magufuli kwa jinsi alivyotusaidia wachimbaji wadogo hasa kwenye kuondoa VAT na ile ya zuio.

Haya yote ni mafanikio yaliyotokana na mkutano wa Mhe. Rais na wadau wa sekta ya madini alioufanya mapema mwezi Januari, 2019 jijini Dar es Salaam,” anaeleza Bw. Bina. Aidha, anaeleza kutokana na mkutano huo mafanikio mengi yamepatikana kutokana na utekelezaji wa maagizo ya Mhe. Rais. Mfano kwa sasa upatikanaji wa maeneo ya uchimbaji hauna urasimu tena na kuwafanya watanzania wengi ambao ni wachimbaji wadogo kuanza kujihusisha na biashara vya madini.

Anafananisha kukumbukwa sawa na mtu aliyekutana na ‘Nyota ya Jaha’ kwani wanaheshimika na wamepata matumaini mapya baada ya kukutana na Rais Magufuli, kueleza kero zao na kisha hatua mbalimbali kuchukuliwa ikiwemo kuondolewa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi ya zuio.

Anaongeza kuwa kada ya wachimbaji wadogo imepata nguvu mpya baada ya kuanzishwa kwa Wizara ya Madini pamoja na Tume ya Madini na kwamba mabadiliko hayo yatawezesha watunga Sera na wasimamizi wa mambo yote yanayohusu madini kuwa katika kapu moja hivyo kuisimamia kwa karibu sekta hiyo.

Pia Bw. Bina anatoa rai kwa vyombo vya habarinchini kuandika sana habari zinazohusu madini kwani yapo mambo mengi ambayo hayafahamiki hususani fursa lukuki zinazopatikana katika madini na kuwasihi kuandika taarifa zilizo sahihi ambazo hazitaichafua nchi kimataifa.

Katika hilo anatoa wito kwa wadau wote katika sekta hiyo kushirikiana kikamilifu na Wizara ili kutatua matatizo ya wachimbaji wadogo, lakini pia kuwataka wachimbaji hao kutambua kuwa mambo yamebadilika na wasiishi tena kimazoea na badala yake walipe mrabaha na wajiepushe na vitendo vya utoroshwaji wa madini ili kusaidia ukuaji wa sekta hiyo.

Rais huyo wa FEMATA anasema lengo la wachimbaji wadogo kwa sasa ni kuondokana na uchimbaji wa kienyeji na kuingia katika uchimbaji wa kisasa na hatimaye kuwa wachimbaji wakubwa wenye kutoa mchango mkubwa kwa jamii na nchi kwa ujumla.

“Hapa nchini kwa sasa madini ndio habari ya mjini, umeona Mhe. Rais katika kikao chetu cha wadau wa madini mwezi Januari mwaka huu alikaa na sisi zaidi ya saa saba ili tuzungumze, na maagizo yote aliyoyatoa mengi yametekelezwa. Mimi najivunia kuwa kwenye sekta hii maana thamani yetu imeonekana, tumeinuliwa tena, tuko juu,” anaeleza Bw. Bina.

**“Hapa nchini kwa sasa madini ndio habari ya mjini, umeona Mhe. Rais katika kikao chetu cha wadau wa madini mwezi Januari mwaka huu alikaa na sisi zaidi ya saa saba ili tuzungumze, na maagizo yote aliyoyatoa mengi yametekelezwa. Mimi najivunia kuwa kwenye sekta hii maana thamani yetu imeonekana, tumeinuliwa tena, tuko juu.”**

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini Tanzania (FEMATA)
**Bw. John Bina.".**



*Mgodi wa Tanzanite, Mirerani*



*Mgodi Wa Wachimbaji Wadogo wa Madini, Nyakavangala, Mkoani Iringa.*

Mapema mwaka huu, katika Mkutano wa Sekta ya Madini uliokutanisha wadau, wachimbaji wadogo, wa kati na wachimbaji wakubwa, wafanyabiashara wa madini pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Madini uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli alisema Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yameiwezesha rasilimali ya madini kuwa mali ya watanzania.

Katika mkutano huo Rais Magufuli alisema marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yamewezsha kurudisha umiliki wa rasilimali madini kwa Watanzania na kuweka usimamizi na udhibiti wa utoroshwaji madini.

Sambamba na hilo ujenzi wa ukuta katika eneo la Madini ya Tanzanite (Mirerani) kumewezesha Tanzania kulinda kwa ukaribu madini ya Tanzanite pia kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini hayo pamoja na ukwepaji kodi.

Mabadiliko makubwa katika Wizara ya Madini yamesaidia ongezeko kubwa la uzalishaji wa madini katika migodi mbalimbali ukiwemo Mgodi wa Almasi wa Mwadui ambao mwaka 2018 ulifikisha uzalishaji wa karati 341,000, ikiwa ni kiasi kikubwa kuzalishwa kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1977 ambapo mgodi huo kiwango cha juu kabisa ilikuwa ni kuzalisha karati 317,000.

Wizara kwa kutambua umuhimu wa wachimbaji wadogo katika kukuza uchumi, imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuwasaidia ikiwemo uanzishwaji wa vituo vya umahiri.

Serikali inajenga vituo saba vya umahiri kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) ili kutoa mafunzo ya nadharia na kuwaongezea ujuzi wachimbaji wadogo katika shughuli zao za uchimbaji utakaowasaidia kuongeza uzalishaji na wenye tija.

Aidha vituo vya umahiri vimelenga katika kutoa mafunzo ya jiolojia hususan katika utafiti wa madini, mafunzo yauongezaji thamani madini, biashara ya madini, uchenjuaji kwa kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira hususanI teknolojia isiyotumia Zebaki.

Vituo vya umahiri vinajengwa katika maeneo ya Mpanda,Bariadi, Handeni, Musoma, Chunya, Songea, Bukoba na jengo la Taaluma katika Chuo cha Madini Dodoma ambalo pia litatumiwa na wachimbaji wanawake.

Mbali na vituo vya umahiri, Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo Wanaozunguka Migodi Mikubwa (Mult-Sector Partnership Initiative MSP), imejenga kituo cha mfano cha Lwamgasa mkoani Geita. Vilevile, Serikali kupitia mradi wake wa SMMRP, imeanza kujenga vituo kama hivyo katika maeneo ya Itumbi Chunya na Katente- Geita na ujenzi unaendelea kwa kasi.



*Naibu Waziri wa Madini, Mhe.Stanslaus Nyongo akikagua shughuli za uchimbaji mdogo wa madini Mkoani Iringa.*

Ili kuhakikisha kuwa wachimbaji wadogo wanapata takwimu za uhakika za kijiolojia zitakazowawezesha kuchimba kwa uhakika, taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) kwa kushirikiana na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) wamefanya utafiti wa kina wa kijiosayansi uliohusisha uchorongaji na ukadiriaji wa mbale (resource) katika maeneo ya wachimbaji wadogo.

Wizara pia imeandaa Mwongozo wa Wachimbaji Madini Wadogo (Guidelines for Small Scale Miners) unaoelezea namna bora ya uchimbaji wa madini na umeshagawiwa kwa walengwa.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, tayari Wizara imetenga maeneo 11 yenye jumla ya ukubwa wa Hekta 38,952 kwa ajili ya uchimbaji mdogo.

Maeneo hayo ni Biharamulo II, Itigi, Kyerwa, D-Reef, Ibinda,Kapanda, Ngapa, Nzega, Kitowelo, Msasa na Matabe.

Ameongeza kuwa, Wizara inaendelea kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo kwa utaratibu wa kuwatembelea wachimbaji hao kufuatilia uwezo wa uzalishaji, soko la Madini wanayochimba pamoja na shughuli za uongezaji thamani madini.

Mafunzo mbalimbali yamekuwa yakitolewa kwa wachimbaji wadogo ambapo jumla ya wachimbaji wadogo 5,303 wamepatiwa mafunzo katika mikoa 15 ambayo ni Manyara, Morogoro, Dodoma, Tanga, Mbeya, Pwani, Shinyanga, Geita, Mara, Katavi, Singida, Dar es Salaam, Mbeya, Lindi na Mtwara.

*Naibu Waziri wa Madini, Mhe.Stanslaus Nyongo akikagua shughuli za uchimbaji mdogo wa madini Mkoani Iringa.*





# STATE MINING CORPORATION







### DRILLING SERVICES FROM STAMICO

STAMICO has been in the mineral exploration drilling business for over the last 35 years in domestic and international exploration activities including the drilling for the Bulyanhulu deposit discovery. Our clients include exploration companies, construction companies, individuals, small scale miners and other groups.

### AIR PERCUSSION/ROTARY DRILLING

STAMICO offers affordable Reverse Circulation (RC)-300m, Rotary Air Blasting (RAB)-150m and Air Core (AC)-30m drilling methods using modern drill Rigs to different clients. Our drilling rigs are wide, compact, efficient and cost effective, capable of drilling indifferent geological terrains.

### DIAMOND CORE DRILLING

STAMICO is offering Diamond Drilling services, at competitive rates. We can drill core in drilling sizes; PQ, HQ, HQ3 (triple tube), NQ sizes with excellent core recoveries in both soft and hard grounds. We utilize modern technologies in our drilling such as down hole surveys and core orientations using Digital tools.

***We can drill different ranges of hole depths from 0- 1,500m deep.***

***Come and acquire our services you will never regret!***

For Quality and affordable Drilling Services please contact us through:

**Managing Director,**
**State Mining Corporation,**
**Plot No: 417/418 United Nations Road.**
**P.O. Box 4958,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**

+255 222 150 029  info@stamico.co.tz  @STAMICO

# USHIRIKISHWAJI WA WAZAWA

## Mfumo Mpya wa Kuchangia Jamii Kuziinua Halmashauri

**Na Mwandishi wetu**



Mageuzi makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika sekta ya madini, kwa kurekebisha Sheria ili kuweka mfumo mpya wa kuratibu utoaji wa huduma kwa jamii (Corprate Social Responsibility),yameanza kuonesha manufaa ikiwemo kuziongezea uwezo Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Utaratibu huo mpya umeainishwa katika Mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika 2017, pamoja na mambo mengine, kuboresha Sheria ya Ushiriki na Uwezeshaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (Local Content) na wajibu wa kampuni za uchimbaji madini kuchangia huduma za kiuchumi na kijamii.

Akizungumza na Jarida la Nchi Yetu hivi karibuni, Kamishna Msaidizi anayeshughulikia eneo la Uwezeshaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini na Wajibu wa Kampuni Kuchangia Huduma za Kijamii, Bw. Terence Ngole, anasema mabadiliko mapya yanawataka wamiliki wa leseni za madini kuandaa mpango wa manunuzi wa miaka mitano wa namna watakavyonunua huduma na bidhaa zinazopatikana hapa nchini.

Aidha, amesema kabla ya Mabadiliko ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, kampuni zilikuwa zikichangia huduma za jamii (Corporate Social Responsibility - CSR) kulingana na jinsi zilivyoona inafaa lakini baada ya mabadiliko hayo, uchangiaji huo uliingizwa kwenye Sheria na Kanuni hivyo kuzielekeza kampuni kutekeleza mipango iliyoridhiwa na jamii inayowazunguka.

Anaongeza kuwa katika kuhakikisha wazawa wanawezeshwa pale ambao huduma au bidhaa husika haipo nchini na hivyo kampuni kulazimika kuiagiza kutoka nje ya nchi, Sheria inaelekeza kampuni za kigeni zitakazoruhusiwa kuagiza lazima ziwe na ubia na kampuni za wazawa, jambo ambalo kwa Sheria ya awali halikuwepo.Aidha, Sheria mpya inamtaka mmiliki wa leseni ya madini ndani ya miezi 12 baada ya kupata leseni, kuwasilisha Mpango wa Ajira na Mafunzo kwa Wazawa ambao utaidhinishwa na Tume ya Madini.

Pia, Sheria inamtaka mmiliki wa leseni kuhakikisha utaalamu na maarifa kuhusu utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini unarithishwa kwa wazawa.

Moja ya eneo jingine muhimu ni kwa wamiliki wa leseni kutakiwa na Sheria hiyo mpya kutenga nafasi za kutosha kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi kutoka katika vyuo vinavyohusiana na Sekta ya Madini hapa nchini ili kuhaulisha ujuzi (skills transfer).



*Mgodi wa dhahabu wa Geita kwa kushirikina na Halmashauri ya Mji wa Geita umejenga madarasa 8 na jengo la utawala la Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Magongo ambavyo vitagharimu shilingi 234.8 milioni.*

## Ushirikishaji Wazawa:

# Mafanikio Yaanza Kuonekana

"Katika kipindi cha kati ya 2015 hadi sasa, Wizara imefanikiwa kusimamia shughuli za CSR katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kuhakikisha wamiliki wa migodi wanatekeleza wajibu wao wa kutoa huduma za Jamii zinazozunguka migodi hiyo kwa mujibu wa makubaliano na vipaumbele vya Jamii inayozunguka migodi hiyo (host community)," anasema Bw. Ngole.

Miongoni mwa mafanikio ya utaratibu huu mpya, ni mfano wa mgodi wa Petra Diamond Mwadui, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, wamejenga lango la kuingilia Hospitali ya Jakaya Kikwete iliyopo wilayani Kishapu kwa thamani ya shilingi milioni 70 za Kitanzania.

Vilevile, Mgodi wa Geita Gold Mine (GGM)umewekeza kwa jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita kupitia miradi ya CSR jumla ya shilingi za Kitanzania 1,143,384,000/= kuezeka majengo 27 ya shule yakijumuisha madarasa, maabara na ofisi za walimu.

Pia, kampuni ya GGM, kwa makubaliano na kutekeleza vipaumbele vya Halmashauri, imejenga kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti na ghala la kuhifadhi magunia 2,020 katika Kata ya Kasota, kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Geita yenye thamani ya shilingi milioni 100 kwa lengo la kuwaongezea kipato wananchi wa Kata hiyo.

Mgodi wa Geita pia umejenga soko la mji wa Geita, ambapo ndani yake kuna soko kuu la kuuza na kununua dhahabu ikiwa ni sehemu ya mchango wao kwa jamii kwa gharama ya shilingi bilioni 3.3 kufuatia vipaumbele vilivyowasilishwa na Halmashauri.

Halikadhalika, mgodi wa GGM kwa kushirikiana na Halmashauri ya mji wa Geita unajenga madarasa nane na jengo la utawala la Shule ya Magongo ambalo litagharimu shilingi milioni 265.

Kwa upande wa utunzaji wa mazingira ya mji wa Geita, mwaka 2018 mgodi na Halmashauri ya mji walikubaliana kujenga mzunguko wa barabara ya Geita – Mwanza kwa gharama ya shilingi milioni 70 na kuweka taa za barabarani kwa shilingi milioni 314 ikiwa ni sehemu ya utoaji wa huduma kwa Jamii.

Baadhi ya huduma hizi haikuwa rahisi kuona matokeo yake na thamani halisi wakati wa utaratibu wa zamani lakini sasa kupitia mfumo wa wazi na shirikishi unaozipa Halmashauri zenyewe nafasi ya kuwasilisha vipaumbele vyao na kukubaliana na wawekezaji husika wa sekta ya madini, matokeo chanya yanaonekana.

*Utekelezaji wa Huduma kwa Jamii (CSR) kwa sekta ya elimu: Ujenzi wa Sekondari J.K. Nyerere Nyamwaga wilayani Tarime umegharimu Dola za Kimarekani 1,347,782 mwaka 2012-2016.*










# SHERIA MPYA SEKTA YA MADINI


043



# ZIJUE FAIDA ZA SHERIA MPYA ZINAZOSIMAMIA SEKTA YA MADINI

Na **Mwandishi wetu**

Dhamira ya dhati ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ya kisimamia rasilimali madini kwa manufaa ya Watanzania, imepata nguvu kupitia Sheria ya Madini, 2010 pamoja na Marekebisho ya Mwaka 2017 na sheria nyingine zilizotungwa mwaka 2017.Ili kuhakikisha rasilimali madini inawanufaisha watanzania, marekebisho ya Sheria yameendelea kuleta tija kwa watanzania kwani vipengele vyote kandamizi vimeondolewa ama kurekebishwa kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mfano, kabla ya Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123, yaliyofanyika Mwaka 2017, wamiliki wa leseni za uchimbaji walkuwa na haki kwa mujibu wa Sheria kusafirisha nje ya nchi bidhaa zote na masalia yanayotokana na uchimbaji, uchakataji na uchenjuaji wa madini.Lakini katika Sheria mpya kupitia kifungu cha (5), imeelekeza kwamba Serikali ndio yenye umiliki wa madini hivyo inaweza kudhibiti madini ya mchimbaji, mchenjuaji, mununuzi na hata muuzaji yeyote hapa nchini.

Kupitia Sheria, Serikali ina haki na dhamna juu ya bidhaa zote na masalia yanayotokana na uchimbaji, uchakataji na uchenjuaji wamadini. Makinikia yote kuanzia sasa ni mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha kwa mujibu wa Sheria ya Madini sura ya 123 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019 hivi sasa mabaki (tailings na mineral ore) inaweza kuuzwa ndani ya nchi kama bidhaa tofauti na ilivyokuwa nyuma.

Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 yaliyofanyika mwaka 2017, yamewezesha kuundwa kwa Tume ya Madini yenye dhamana ya kusimamia shughuli za madini.

Tume ya Madini ni Mamlaka ya Leseni na Udhibiti wa shughuli zote zinazofanyika kaika sekta ya Madini. Kwa mujibu wa Sheria, Tume ya Madini ina uwezo wa kushitaki au kushitakiwa. Vilevile inayo mamlaka ya kumiliki mali na kubuni vyanzo vya mapato yake.

Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 yaliyofanyika mwaka 2017, yameweka utaratibu mahsusi kuwa madini yakisha chimbwa sharti yatambuliwe na kupimwa kwa ushirikiano wa Afisa Migodi Mkazi na Maafisa wa Serikali pamoja na mchimbaji husika.

Marekebisho ya Sheria yamefuta iliyokwa Wakala wa Jiolojia Tanzania na kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kijiolojia iitwayo'Geological Survey of Tanzania (GST)'.

Kwa mujibu wa Sheria, Taasisi GST imepewa dhamana ya kusimamia shughuli zote za utafiti wa kijiolojia nchini, pamoja na kusimamia shughuli za utafiti wa madini.

Aidha kwa sasa Kampuni za Utafiti na Uchimbaji Madini (Mining and Exploration Companies) zinalazimika kuwasilisha GST taarifa na kanzidata zao kuhusu utafiti na uchimbaji.

Faida nyingine ya uwepo wa Sheria mpya ya Madini ni kuanzishwa kwa utaratibu mpya wa ushirikishaji wa jamii zinazozunguka shughuli za uchimbaji madini.



*Baadhi ya Madini mbalimbali yanayopatikana Tanzania.*



Kwa sasa utaratibu wa uchangiaji wa huduma za jamii (CSR) umekuwa shirikishi kati ya kampuni za madini na jamii husika kupitia Serikali zao za Vijiji, Miji au Wilaya.

Utaratibu huu umewawezesha wananchi kushiriki moja kwa moja na kujipangia miradi ya maendeleo ambayo ndiyo kipaumbele kwao kuingizwa katika mipango mikakati ya kampuni za madini tofauti na ilivyokuwa kabla yamabadiliko ya Sheria ambapo kampuni zilikuwa zinajiamulia zichangie vipi jamii bila hata kuangalia vipaubele vya jamii husika.

Faida nyingine ya Sheria mpya kwa Watanzania ni kwamba imeweka masharti na utaratibu unaohakikisha kuwa shughuli zote za uchimbaji madini katika nchi zinazingatia misingi inayolinda mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191.

Aidha, sheria inaweka mkazo kwa watanznia kupewa kipaumbele katika ajira na eneo lolote ambalo litakosa mzawa mwenye taaluma hiyo, basi ni lazima kuwe na mpango wa urithishaji (Succession Plan).

Vilevile Sheria inasisitiza mafunzo na kuhawilisha teknolojia (technology transfer) katika sekta ya Madini.

Sheria imeelekeza wamiliki wa leseni za uchimbaji kutoa kipaumbele kwa bidhaa zinazozalishwa au kupatikana nchini na pia kupata huduma kutoka kwa kampuni za watanzania, mfano huduma za kibenki, kisheria , bima na kadlika.

Uzuri mwingine wa mabadiliko ya Sheria ni kwamba mikataba yote nchi itayoingiwa ni lazima izingatie Sheria ya Mwaka 2017 kuhusu Ukuu wa Nchi katika Raslimali Madini iitwayo 'The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignity) Act,2017', ambayo inasisitiza kwamba makubaliano yote ni lazima yazingatie maslahi ya nchi kama Mmiliki halali wa Rasilimali Madini yanayovunwa.

Waombaji na wamiliki wa wa leseni za uchimbaji wa madini wameelekezwa na Sheria kuwasilisha Tume ya Madini kiapo cha uadilifu ikiwemo kukubaliana na sharti la Serikali kuwa na asilimia 16 ya hisa huru kwa kila leseni ya uchimbaji madini.

Sambamba na mabadiliko hayo ya Sheria ya Madini, Wizara pia imetengeneza Kanuni na Miongozo mahsusi ili kusaidia utekelezaji wa Sheria katika kuleta mabadiliko chanya kwenye sekta ya madini.

Miongoni mwa Kanuni ni Kanuni mpya za Udhibiti wa Eneo la Mirereani, 2019 ambazo lengo lake ni kufanya usimamizi wa eneola Mirerani uendane na mabadiliko ya Sheria ya Madini, pamoja na kuhuisha tozo mbalimbali katika usimamizi na udhibiti baada ya eneo hilo kuzungushiwa ukuta.

Kanuni nyingine ni zile za Biashara ya Madini ya Almasi, 2019, ambazo lengo lake ni kusimamia biashara ya madini ya Almasi nchini.

Kanuni hizi zinaweka utaratibu wa kuuza na kununua madini ya Almasi ambako kunaiwezesha Serikali kupata mrabaha na tozo mbalimbali kutokana na mauzo ya madini hayo.

Aidha Kanuni nyingine ni zile zijulikanazo kama Kanuni za Madini (Kiapo cha Uadilifu), 2018, ambazo zimeweka utaratibu wa kuwailisha kiapo cha uadilifu kwa wanaofanya shughuli za uchimbaji madini nchini.

Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Tume ya Madini imetunga pia Mwongozo wa Kuhakiki Uongezaji Thamani Madini au Miamba kabla ya Madini Kusafirishwa Nje ya Nchi (The Mining (Mineral Value Addition) Guidelines, 2019).

Lengo la kutunga Mwongozo huu ni kuweka utaratibu mzuri wa uongezaji thamani madini kabla ya kusafirisha kwenda nje ya nchi.

Utaratibu huu unaweka viwango vya uongezaji thamani kwa kila madini na miamba kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi.

Sambamba na mwongozo huo, Kanuni za Madini (Ushirikishwaji wa Huduma na Bidhaa za Watanzania), 2018 zilitungwa kwa lengo la kusimamia na kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji madini nchini zinashirikisha huduma na bidhaa zinazozalishwa na Watanzania.

Kanuni zinaweka utaratibu wa kuajiri Watanzania katika kampuni za uchimbaji madini na kutumia huduma na bidhaa zinazolishwa na watanzania nchini.

Kwa upande mwingine, Wizara imetunga Kanuni za Madini (Biashara ya Madini na Makinikia), 2018 kwa lengo lakusimamia na kuhakikisha shughuli za uchimbaji madini nchini zinatenganisha madini na makinikia yatokanayo na uchimbaji huo.

Kanuni hizi zinaweka utaratibu unaozuia usafirishaji wa makinikia nje ya nchi, kwa lengo la kuhamasisha shughuli zote za uchenjuaji wa madini ghafi kufanyika ndani ya nchi.Unapozungumzia umuhimu wa Kanuni mpya zinazoiwezesha Sheria mpya ya Madini kufanya kazi, huwezi kuacha kuzungumzia Kanuni za Madini (Uongezaji Thamani Madini), 2018, Kanuni hizi zinaweka utaratibu wa uongezaji thamani madini na taratabu za uchenjuaji wa madini ghafi nchini.Utaratibu wa kuongeza thamani unalenga kuhamasisha ili shughuli zote za uchenjuaji wa madini ghafi zinafanyika ndani ya nchi ili kuyaongezea madini yote thamani kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

Kanuni nyingine ni zile za Madini (Haki Madini), 2018 ambazo zinasimamia na kuhakikisha kuwa shughuli za utoaji wa leseni za utafiti au uchimbaji madini nchini zinazingatia masharti na haki.Wizara ya Madini katika kuhakikisha inasimamia rasilimali madini kwa manufaa ya watanzania, imetunga pia kanuni za Utafiti wa Kijiolojia, 2018, Kanuni za Ukaguzi na Uchunguzi wa Migodi, 2018, Kanuni za Madini Mionzi, 2018, pamoja na Kanuni za Uwazi na Uwajibikaji katika Sekta ya Madini, 2019.

Faida hizi za jumla kiudhibiti na mafanikio mengi yaliyoanza kuonekana kama yanavyoainishwa katika makala mbalimbali zilizomo katika jarida hili vinatukumbusha jambo moja muhimu; Tanzania si maskini lakini tukithubutu, tunaweza kuifanya sekta ya madini iitajirishe nchi yetu.




# TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA - GST



**TUMIA TAARIFA ZA JIOSAYANSI ZINAZOZALISHWA KUPITIA TAFITI ZINAZOFANYWA NA TAASISI YA JIOLOJIA NA UTAFITI WA MADINI TANZANIA (GST) KWA UTAFUTAJI NA UCHENJUAJI WA MADINI WENYE TIJA.**







ANWANI YETU:

**Mtendaji Mkuu,**
**Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania,**
**S.L.P 903,**
**DODOMA.**

## KWA MAWASILIANO ZAIDI ,WASILIANA NA:

**Simu namba:** +255 26 2323020
**Nukushi:** +255 26 2323020

**Barua pepe:** madini.do@gst.go.tz

**Tovuti:** http:www.gst.go.tz



# GEITA
# MJI WA DHAHABU

## Kioo cha Faida ya Mageuzi Sekta ya Madini

Na **Mwandishi wetu**

Tanzania inasifika Afrika na duniani kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii ukiwemo Mlima mrefu kuliko yote Afrika, Mlima Kilimanjaro, uliopo katika mkoa wa Kilimanjaro, lakini linapokuja suala la madini nchini Tanzania,jina la Geita lazima litasikika.

Geita au baadhi wanavyoubatiza jina kuwa Mkoa wa Dhahabu (Place of Gold) ni mkoa maarufu kwa utajiri wa rasilimali madini hususan dhahabu.


Mkoa huu ulianzishwa rasmi kwa Tangazo la Serikali namba 72 la Machi 2, 2012, na kuzinduliwa rasmi Novemba 08, 2013 na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mkoa ulitokana na sehemu ya Mikoa ya Mwanza, Kagera na mkoa wa Shinyanga.Geita ni miongoni ya mikoa ambayo ipo ndani ya maeneo ambayo kijiolojia duniani kote yanafahamika kwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini dhahabu (Greenstone Belts).

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel anauelezea Mkoa wa Geita kuwa kioo cha mafanikio katika mageuzi yanayoendelea kutekelezwa na Serikali katika sekta ya madini.

Akizungumza hivi karibuni na Jarida la Nchi Yetu, , Mhandisi Robert Gabriel anauelezea Mkoa wa Geita kuwa kioo cha mafanikio katika mageuzi yanayoendelea pia ni kutokana na nia mpya ya Uongozi wa Mkoa.

Aidha, anasema kuwa wilaya zote tano za mkoa ambazo ni: Geita, Chato, Bukombe, Mbogwe na Nyang'wale zina hazina ya madini ya dhahabu na kwamba shughuli za uchimbaji madini zimewapa wananchi fursa za biashara na ajira. Lakini pia Mkoa kupata mapato na kuchangia katika pato la Taifa.



# GGM YAONGOZA KUCHANGIA MAPATO

Tofauti ya Mkoa wa Geita na mikoa mingine inayozalisha madini, ni kiwango kikubwa cha uzalishaji wa dhahabu kinachochangiwa na uwepo wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) ambao ndio unaongoza kwa kutoa mchango mkubwa kwenye makusanyo ya mapato kutoka katika sekta ya madini nchini.

Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi mwaka huu, 2019 mgodi huo umechangina shilingi bilioni 98 kati ya shilingi bilioni 244 zilizokusanywa katika sekta ya madini, sawa na asilimia 40. Mgodi wa GGM ambao unaongoza kwa uzalishaji wa dhahabu hapa nchini, unaipatia Serikali mapato makubwa kutokana na kodi na tozo mbalimbali lakini pia umewapatia watanzania wengi ajira rasmi na zisizo rasmi.

Kutokana na wingi wa madini,kumekuwa na shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo idadi kubwa ya wachimbaji wadogo na wa kati na hivyo kufanya mkoa wa Geita kuwa na vituo vingi vya uchenjuaji wa madini ukilinganisha na sehemu nyingine yoyote nchini. Mkoa wa Geita peke yake una vituo 31 vya uchenjuaji (Elution Plants) kati ya vituo 100 ambayo ni takribani asilimia 24 ya vituo vyote vilivyopo nchini. Vilevile, kati ya mashine 639 za uchenjuaji (CIP, CIL na VAT Leaching) nchini, mashine 173 ziko mkoani Geita ambazo ni sawa na asilimia 27.

Mkoa wa Geita ndio ulikuwa wa kwanza kutekeleza agizo la Serikali la kuhakikisha mitambo ya uchenjuaji wa dhahabu haiwekwi nje ya mkoa ambako madini yanazalishwa. Mkoa ulitenga eneo maalum kwa ajili hiyo. Utekelezaji wa agizo hilo uliofuatiwa na Mkoa wa Geita kupokea wawekezaji wengi waliojenga mitambo yao umesaidia kupunguza utoroshaji wa Madi ni ambapo itasaidia Serikali kuongeza mapato.

## GEITA YAANZA NA SOKO KUU LA MADINI

Mhandisi Gabriel anaeleza kuwa katika soko hilo ambalo limefungwa kamera za kisasa za CCTV kwa ajili ya kuimarisha ulinzi, kuna ofisi mbalimbali za kusimamia biashara na kukusanya tozo mbalimbali za Serikali, ofisi za Tume ya Madini, Idara ya Uhamiaji, Halmashauri na Jeshi la Polisi kwa ajili ya ulinzi na usalama na utoaji wa huduma nyingine.

Kwa upande wake, Afisa Madini wa Mkoa, Bw. Daniel Mapunda anaeleza kuwa uanzishwaji wa soko hilo umepunguza utoroshwaji wa madini kutoka nje ya mkoa na kwa sasa Serikali inapata takwimu sahihi za uzalishaji na uuzaji tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma.

Mapunda ameongeza kuwa soko hilo limesaidia kuongezeka kwa vibali vya kusafirishia dhahabu nje ya nchi ambapo hutolewa kwa kulipia dola za kimarekani 100 kwa kimoja na hivyo kusaidia kujua takwimu za dhahabu iliyouzwa nje ya nchi.

Kwa upande wao, Wafanyabiashara Juma Kinyagata wa Kampuni ya Makono Manganyala Kaniki na Peter Moses wa kampuni ya Paul Mariganya, wanaeleza kuwa kuanzishwa kwa soko hilo kumewafanya watambuliwe rasmi na Serikali jambo ambalo linafanya wafahamike zaidi na kuwaongezea heshima na uaminifu kwa wateja wao.

Tangu soko hilo lizunduliwe rasmi na Waziri Mkuu mwezi Machi 2019, jumla ya kilo 283.7 za dhahabu zenye thamani ya shilingi bilioni 23.7 ziliuzwa sokoni hapo. Mauzo ya dhahabu katika soko hilo yameifanya Serikali kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **1,659,648,571.97** (Kuanzia Machi 17 hadi Mei 16, 2019) kutokana na tozo ya Mrabaha (Royalty) na tozo ya ukaguzi (CIF)





Kwa mujibu wa Mhandisi Gabriel, mchakato wa kuanzisha soko hilo ulianza rasmi mwezi Januari, 2019 kufuatia agizo la Rais Dkt. John Pombe Magufuli, ambapo Mkuu huyo wa Mkoa aliona soko hilo ni fursa kwa Mkoa wa Geita na wakaamua kubadili jengo lililokuwa linajengwa kuwa soko la kawaida kuwa soko la madini.

Soko hilo lililozinduliwa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa tarehe 17, Machi, 2019, lipo katika miundombinu inayomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Akielezea juu ya mfumo wa uendeshaji wa soko hilo, Mhandisi Gabriel anasema kuwa shughuli za kibishara katika soko zimerahisishwa ili kuondoa urasimiu ambapo ndani ya soko hili kuna taasisi za kifedha kama benki za CRDB, Azania na NMB kwa ajili ya kurahisisha miamala ya fedha taslimu na zisizo taslimu.

“Ndani ya soko hili kuna wanunuzi wakubwa wa dhahabu wapatao 14 na kwa sasa ujenzi wa ofisi zaidi kwa ajili ya wanunuzi wakubwa wa dhahabu zinaendelea kujengwa ili kukidhi mahitaji ya wanunuzi wote 18 waliopo Mkoani Geita kwa sasa,” anasema RC Gabriel.





*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Kassim Majaliwa akiangalia Madini ya Dhahabu mara baada ya uzinduzi wa Soko la Madini Mkoani Geita, Machi 17, 2019.*




# JICHO LA WANAHABARI KATIKA MABADILIKO SEKTA YA MADINI TANZANIA

Na **Mwandishi Maalum**

Mwaka 2017, Bunge lilifanya marekebisho katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 7 ya mwaka 2017.

Aidha, baadaye iliundwa Wizara mpya ya Madini. Wizara hiyo ilianzishwa baada ya kuvunjwa kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini kupitia Hati ya Majukumu ya Wizara "Instrument" Na. 144 iliyotolewa mwaka 2016 na Marekebisho yake ya Oktoba 7, 2017, lengo likiwa ni kuhakikisha kwamba rasilimali madini zinasimamiwa vyema ili ziwanufaishe watanzania wote.

Bunge pia lilishapitisha sheria mbili zinazohusu ukuu wa Tanzania kama nchi katika kumiliki raslimali zake za madini na uwezo wa kujadiliana na kurekebisha vipengele vyenye masharti hasi katika sekta ya madini.

Miongoni mwa mambo mapya yaliyoletwa na mabadiliko hayo mbalimbali ya sheria ni pamoja na kutambua na kuweka umiliki wa rasilimali za madini kwa wananchi chini ya usimamizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi, kuweka ulinzi na usimamizi mahsusi wa maeneo yote ya uchimbaji wa madini, kuweka utaratibu wa Bunge kufanya mapitio mikataba ya uchimbaji na uendelezaji wa madini, kutungwa kwa Kanuni za Madini (Biashara ya Madini na Makinikia) za 2018 na kutungwa kwa Kanuni za Madini kuhusu Ushirikishwaji wa Watanzania na Bidhaa za Ndani za 2018.

Mabadiliko mengine ni kuboresha utaratibu mzuri wa ulipaji wa mrabaha wa Serikali ambao uliongezeka kutoka asilimia nne na kuwa asilimia sita ya bei ya madini ghafi kwa madini ya metali na vito na kuanzishwa kwa ada ya ukaguzi wa madini ya kiasi cha asilimia moja, kuweka utaratibu wa mafunzo na kuhamisha teknolojia ya uchimbaji wa madini (Local Content), kuanzisha Tume ya Madini, kuweka zuio la kutoa au kuondoa madini katika eneo la migodi na kuzuia uuzaji na usafirishaji wa madini ambayo hayajaongezwa thamani.

Kabla ya mabadiliko haya kulikuwa na malalamiko mengi miongoni mwa wanasiasa, wachimbaji wenyewe wa madini, wananchi na waandishi wa habari ambao kwa kiasi kikubwa waliandika katika vyombo vya habari kutaka hatua zichukuliwe ili rasilimali hiyo iwe na manufaa kwa Taifa.Baada ya mabadiliko ya Sheria kufanyika, baadhi ya Wahariri na waandishi wa habari wameongea na Jarida la Nchi Yetu na kutoa maoni yao juu sekta ya madini.

Hamis Kibari, Mhariri wa Makala wa gazeti la HabariLeo, anasema kuwa mabadiliko yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ni hatua kubwa ya kuifanya nchi inufaike na madini yake.

Kibari anatolea mfano wa zuio la kusafirisha kaboni nje ya mkoa limesaidia kuongeza kiwango cha madini kinachopatIkana katika mkoa husika na kuiwezesha Wizara kupata takwimu sahihi za madini yanayopatikana.

"Kuzuia kaboni hasa katika mikoa yenye madini mengi kama Mkoa wa Geita kumeleta mabadiliko makubwa kwa muda mfupi sana kwani kiwango cha madini yanayopatikana kimeongezeka karibu mara tatu ya kiwango cha zamani," anaeleza.

Kibari anafananisha ongezeko kiwango cha madini kinachopatikana kwa sasa katika machimbo mbalimbali kama Mirerani na Geita na kauli ambayo imekuwa ikitamkwa mara kwa mara na Rasi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwamba Tanzania hii ni tajiri kutokana na rasilimali ilizo nazo.

"Najua bado tunaibiwa lakini tupo katika hatua nzuri ya kufaidika na rasilimali zetu" anasema.

Naamini kutokana na hatua ambazo Serikali inaendelea kuchua baada ya miaka 10 tutakuwa vizuri," anaeleza Kibari.

Aidha, anatoa wito kwa Wizara ya Madini na taasisi zake kuendelea kusimamia vema rasilimali madini ili nchi inufaike zaidi na rasilimali hizo.

Kwa upande wake, Mahariri wa gazeti la Jamhuri ambaye pia ni Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile anasema uamuzi uliofanywa na Serikali kupeleka Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na hatimaye Bunge kufanya mabadiliko ni hatua kubwa ambayo yameweka usawa kwani kabla ya hapo wawekezaji wa kigeni walionekana kupendelewa zaidi kuliko wazawa.

Balile anaelezea matumaini yake kwa Wizara ya Madini kutokana na Wizara hiyo kuimarisha usimamizi katika sekta ya madini na kwamba pamoja na jitihada za kuanzisha masoko ya madini hapa hapa nchini, ni muhimu pia kutafuta masoko ya nje.

"Kwa sasa tunaona jinsi Wizara inavyosimamia vizuri sekta ya madini nchini lakini pamoja na juhudi hizo, nashauri Wizara itoe elimu kwa waandishi wa habari juu ya mabadiliko hayo ili kuwaongezea uelewa wa sekta hii muhimu kwa taifa," anaeleza Balile.

Mwandishi wa magazeti ya The Citizen na Mwananchi, Joseph Lyimo kutoka mkoa wa Manyara, anaeleza kuwa mabadiliko ya Sheria wamewahamasisha wachimbaji na wafanyabiashara ya madini ambao wanaona sekta ya madini inatoa matumaini kwa watanzania kupinga juhudi za Serikali na kuishauri Wizara kuendelea kusimamia Sheria na taratibu kwa ajili ya maslahi ya watanzania, badala ya kusikiliza watu wachache ambao walikuwa wananufaika na wizi wa madini.

Ili kuboresha na kuifanya sekta hiyo iwanufaishe zaidi watanzania, Mwandishi huyo ambaye pia amefanya kazi katika vyombo mbalimbali vya habari nchini, anatoa ushauri kwa watanzania kuingia kwa wingi kwenye biashara ya madini ili rasilimali hiyo iwanufaishe na pia kuwataka wawe walinzi kudhibiti wizi na utoroshaji wa raslimali hiyo.

Kutokana na mwamko mkubwa wa ulipaji kodi na mrabaha kutoka kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini, Lyimo anatoa ushauri kwa Wizara ya Madini kuongeza idadi ya Wathamini Madini hususan katika machimbo ya Tanzanite yaliliyopo Mirerani mkoani Manyara kwa lengo la kupunguza foleni ya wachimbaji kusubiri kufanyiwa uthamini wa madini yao ili walipie tozo na mrabaha.

"Wathamini wapo wachache hasa kwenye madini ya Tanzanite na hivyo kusababisha wachimbaji na wafanyabiashara kushindwa kuzungusha mitaji yao vizuri kwa sababu wanakaa muda mrefu kusubiri madini kuthaminiwa," anaeleza Lyimo ambaye kwa muda mrefu amekuwa akiandika habari kuhusu machimbo ya madini ya Tanzanite.

Kwa upande wake, Mhariri Mkongwe katika tasnia ya habari, Joseph Kulangwa anasema mabadiliko yaliyofanyika yameiweka sekta ya madini mikononi mwa wananchi tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo wawekezaji wa kigeni walikuwa na nguvu kubwa.

"Kabla ya ukuta pale Mirerani ilikuwa ni kama Shamba la Bibi maana watu walikuwa wanaiba na kuchimba kiholela na kwenda kuuza Kenya jambo ambalo lilikuwa lina athari kubwa kwa uchumi wa Tanzania.

Lakini sasa tunaona hali imekuwa bora zaidi, umewekwa utaratibu mzuri na madini yanaongezwa thamani," anaeleza Kulangwa. Aidha, Kulangwa anasema pamoja na kwamba kuna maboresho makubwa ikiwemo kujengwa ukuta wa Mirerani, bado kuna watu wanajitokeza.



# DUNIA ILIVYOFUATILIA MAGEUZI YA JPM SEKTA YA MADINI



## Na Mwandishi Wetu

TANGU Rais John Pombe Magufuli alipoahidi katika kampeni zake na hatimaye kuanza kutekeleza mageuzi mbalimbali katika sekta ya madini, watafiti, wanasiasa na wasomi mbalimbali duniani wameyachambua au kuyapokea mageuzi hayo kwa namna mbalimbali. Utafiti uliofanywa na jopo la timu ya NCHI YETU Tanzania unaonesha kuwa pamoja na kuwepo walioyapokea mageuzi hayo kwa mtazamo hasi kutokana na kuwa wahanga wa mfumo mpya wa kuhakikisha Watanzania wanafaidika zaidi na madini yao, wasomi, wanasiasa na watafiti wengi duniani wameitaja Tanzania kama mfano bora katika kusimamia nchi kufaidika na raslimali zake.

Nia hii ya wazi imewagusa wananchi wa Tanzania lakini pia wachambuzi kutoka mataifa mbalimbali duniani na kuizungumzia au hata kuitetea dhamira hiyo kila ilipotaka kupotoshwa.

Ndio maana baada ya jarida la African Arguments toleo la Julai, 2017 kuchapisha makala iliyokuwa na anuani ya (**"Tanzania: Magufuli's Mining Reforms are a Masterclass in Political Manoeuvring"**) ikikosoa mageuzi yanayoendelea, wasomaji wengi kutoka kote duniani waliungana na msimamo wa Tanzania kutetea rasilimali zake za madini.

"Magufuli ni kiongozi anayetazama mbali, anajua jinsi ya kusimamia raslimali za nchi yake ili ziwanufaishe watu wake. Sisi tunaoishi nchi za Ulaya tunafahamu jinsi Mataifa ya huku yanavyoulinda uchumi wao," alisema msomaji mmoja kutoka nchi za Ulaya na mwingine akaongeza: "Tuache kasumba za kimagharibi, anachokifanya Magufuli nchini Tanzania ndicho kinachotakiwa. Madini lazima yawanufaishe wananchi wa maeneo husika kwanza kabla ya wengine. Magufuli aendelee na mageuzi. Safi."

### Mageuzi Yake Yawalenga Wengi

Katika makala iliyoandikwa "Magufuli as been President for Two Years: How He's Changing Tanzania" na kuchapishwa katika jarida la The Conversation, mwandishi Dkt. Dan Paget kutoka Chuo Kikuu cha Oxford anatoa maono yenye kuhusu falsafa za Magufuli katika sekta ya madini.

Anazungumzia sheria mpya zilivyotungwa, anazungumzia taasisi zilizowekwa na anazungumzia wasiwasi wa wawekezaji baada ya mageuzi hayo. Lakini anakwenda mbali kwa kuweka maoni yake kuhusu mageuzi yote haya kuwa Rais Magufuli anazingatia kujali maslahi ya watu wake na ni mtu wa maadili.

Anaandika: *"But the definitive feature of Magufuli's first two years has been a talent for pursuing his programme of reform while pursuing domestic popularity at the same time….Perhaps more than any other president since Tanzania's founding father, Julius Nyerere, Magufuli is seen as a man of integrity."*

### Stephen Sucker na Mafanikio ya JPM.

Akiendesha kipindi cha mahojiano yaliyohusu Tanzania, mtangazaji mashuhuri wa kipindi cha BBC Hard Talk, Stephen Sucker, alieleza jinsi sera za kuzibana kampuni kubwa za madini zilivyosaidia Tanzania kuongeza mapato yake.

Kipindi hicho kilichotazamwa na mamilioni ya watu duniani, kiliwashangaza wengi kwa jinsi mwanahabari huyo alivyofanya utafiti kuhusu mafanikio ya sera nyingi za kimageuzi za Rais Magufuli ikiwemo utungaji wa sheria mpya, mageuzi ya kitaasisi lakini pia mapambano dhidi ya rushwa.... *Inaendelea Ukurasa wa 45*





## WACHIMBAJI WADOGO WAGUSWA

Katika makala iliyochapishwa Machi, 2019 katika jarida la mtandaoni la nchini Nigeria (http://venturesafrica.com/about/) chini ya kichwa cha habari kisemacho: "Tanzania Eases Indigenous Regulations in Mining Sector Reforms," mtandao huo unachambua Kanuni mpya za Madini nchini kuwa zitawasaidia wachimbaji wadogo.

"Local miners, most of whom cannot afford things such as machinery, have welcomed the amendment, saying it will make the mining industry vibrant.

"Many local companies, be they contractors, subcontractors, licensees, do not have the capital and capacity needed to bring about development in the mining activities," one of the miners in Tanzania, Mbwaike Mahyenga said."

Makala hiyo inaeleza maoni ya wachimbaji nchini Tanzania wakifurahia Kanuni mpya za Madini, za Mwaka 2018 zilizotolewa mwaka jana ambazo zimeshusha ulazima wa Mtanzania kumiliki hisa nyingi (kwa kuanzia asilimia 51) katika sekta ya madini hadi kuwa asilimia 20.

Aidha uchambuzi wa mtandao huo pia umepongeza Kanuni kuziruhusu na kuziwekea ushiriki benki za Kitanzania katika kushiriki kuhifadhi fedha za madini, jambo ambalo limeelezwa kuwa litazisaidia benki nyingi za hapa nchini.

"Economists believe it is a good move since the new regulations will allow more local banks which are not wholly Tanzanian owned to provide services to the sector."

Mafanikio haya ya Tanzania kusukuma ajenda ya wazawa kunufaika yameanza pia kuwa na mwangwi katika baadhi ya Mataifa ya Afrika ambako nako mikataba mbalimbali imeanza kupitiwa kwa lengo la kubadilisha vifungu vyenye masharti hasi.

Pamoja na baadhi ya watu kuwa na hisia kuwa mageuzi haya yangewaondoa wawekezaji, hali imekuwa tofauti, tayari Tanzania imeshaanza mazungumzo na kampuni mbalimbali kubwa za madini na kufikia makubaliano ikiwemo Acacia na Tanzanite One kuhakikisha Serikali inafaidika zaidi kwa niaba ya wananchi.

Aidha, mchango wa jumla wa sekta ya madini umekua. Ukuaji wa Sekta ya madini ulikua kwa kasi na kuongezeka kufika asilimia 18 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 12 mwaka 2015/16 na makusanyo ya maduhuli yameongezeka kutoka lengo la TZS bilioni 194 hadi TZS Bilioni 301 mwaka 2017/18.

Ni muhimu kwa viongozi wote wa umma na wadau kuendelea kushirikiana kusimamia maono haya na mageuzi haya ili Taifa lizidi kupata mapato yake yatakayosaidia kubadili maisha ya watanzania kwa kuwapatia huduma bora zaidi za kijamii.



# TUME YA MADINI YAVUKA LENGO UKUSANYAJI WA MADUHULI

Na **Mwandishi wetu**

Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017 yaliyoweka msingi wa udhibiti wa rasilimali madini, yamesaidia kuongezeka mapato ya Serikali yatokanayo na shughuli za madini. Marekebisho hayo ambayo pamoja na mambo mengine yaliunda Tume ya Madini, yamesaidia kujenga msingi wa kitaasisi ambapo sasa yameongeza makusanyo ya maduhuli ya Madini nchini.

Kwa mfano, katika Bajeti ya mwaka huu 2018/19, lengo ni kukusanya maduhuli yanayofikia TZS bilioni 310. Hadi kufikia Machi, 2019 Tume ilishakusanya takribani TZS bilioni 244.

Kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Profesa Shukrani Manya, mafanikio hayo yametokana na maelekezo na miongozo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli ya kufanya marekebisho ya Sheria ili kuhakikisha vipengele kandamizi vinaondolewa kwa maslahi ya Watanzania.

Anasema Tume ya Madini kwa sasa imepewa nguvu ya kisheria kusimamia utoaji wa leseni, utafiti, uchimbaji, uchenjuaji pamoja na biashara ya madini kwa ujumla.

Majukumu mengine ya Tume ya Madini ni kufanya ukaguzi wa migodi na uchunguzi juu ya masuala ya afya na usalama kuhusiana na shughuli zote zinazofanyika migodini, kwa lengo la kuhakikisha uchimbaji unakua salama.

Aidha Tume ya Madini inashughulika pia na kufuatilia na kukagua shughuli za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi pamoja na uchenjuaji madini.

Profesa Manya anaelezea zaidi kuwa tangu kuanzishwa kwa Tume ya Madini mwezi Aprili, 2017, jumla ya maombi ya leseni 11,537 yameidhinishwa na Tume kwa ajili ya kupewa leseni za utafutaji wa madini, uchimbaji mdogo, uchimbaji wa kati, uchenjuaji wa madini pamoja na biashara ya madini hadi kufikia Machi, 2019.

Kati ya hizo leseni 8,586 ni za wachimbaji wadogo, 31 za uchenjuaji madini, 689 za biashara kubwa ya madini, pamoja na 1,324 za biashara ndogo ya madini.

Tume hiyo pia imetoa leseni 58 kwa ajili ya uchimbaji- wa kati wa madini, leseni 846 za utafutaji wa madini pamoja na leseni tatu za uchimbaji mkubwa ziko katika hatua za mwisho ili kutolewa.

Kwa mujibu wa Tume ya Madini, utoaji wa leseni mpya za uchimbaji wa kati wa madini, katika kipindi cha miaka mitano ijayo kutawezesha kuchimbwa kwa madini ambayo hayakuwahi kuchimbwa hapo awali.

Madini hayo mapya yanayotarajiwa kuzalishwa ni pamoja na madini ya kinywe (graphite), madini mazito kama zircon, ilmenite, rutile pamoja na Rare Earth Elements (REE). Madini ya graphite yanapatikana katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Lindi pamoja na Mtwara wakati madini ya Rare Earth elements yanapatikana katika mkoa wa Songwe.

Tume pia husimamia upatikanaji wa takwimu za uzalisahaji madini migodini, kuthaminisha madini ili kupata thamani halisi ya madini yaliyozalishwa kabla ya kuuzwa kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. Vilevile, Tume ya Madini hutoa bei elekezi kwa madini yanayozalishwa nchini ikilinganishwa na bei katika soko la kimataifa.


Tangu mwezi Novemba, 2018, Tume imeendelea kutoa bei elekezi ya madini kila mwezi, hatua ambayo imewasaidia wachimbaji wadogo wanaouza madini katika viwanda ambao walikua wakipunjwa na wenye viwanda kupanga bei waitakayo wao.

Tume ya Madini pia ina jukumu la kukagua gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa na ya kati kwa lengo la kukusanya taarifa sahihi za kodi na kuziwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na mamlaka nyingine kwa lengo la kuepusha udanganyifu unaoweza kufanywa na Kampuni kubwa za kimataifa zinazokuja kuwekeza katika sekta ya madini.

Kwa kuwa Serikali imeendelea kuchukua hatua za kudhibiti utoroshaji wa madini pamoja na ukwepaji kodi, Tume ya Madini imeweka udhibiti mkubwa katika viwanja vikubwa vya ndege, mipakani pamoja na bandarini, ili kuwezesha rasilimali hiyo muhimu kuwanufaisha Watanzania.

Tume ya Madini iliundwa kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010, pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2017 ili kusimamia na kuratibu kikamilifu utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Madini kwa maslahi ya Taifa. Serikali itaendelea kuimarisha Tume ili itekeleze majukumu yake.





# GST YAKAMILISHA TAFITI KUWAINUA WACHIMBAJI MADINI

Na **Mwandishi Wetu.**

Jitihada za Serikali kuhakikisha rasilimali madini zinawanufaisha watanzania, zimeendelea kudhihirika ambapo miongoni mwa mikakati mahsusi ni kuimarisha Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST).

Taasisi hii sio tu ni muhimu kwa Wizara bali kwa nchi kwa kuwa ndiyo yenye dhamana ya kufanya utafiti kuhusu miamba na madini kwa lengo la kutambua viashiria vya madini kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini.

Kwa mujibu wa Kaimu Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST), Bibi. Yokberth Myumbilwa, GST imepewa mamlaka ya kukusanya taaarifa kutoka kwenye makampuni ya utafiti na uchimbaji wa madini na kuzihifadhi kwenye kanzi data.

Amesema kuwa ukusanyaji wa taarifa na kuziweka katika kanzidata ni muhimu kwa nchi ili kuhakiki usahihi wa taarifa za utafiti na uchimbaji ili kuweza kuepuka udanganyifu kwa Serikali na wafadhili wa miradi ya madini.

Bibi. Myumbilwa anaeleza kuwa, GST ina jukumu la kuratibu na kusimamia jinsi ya kupunguza madhara ya majanga yote ya asili yatokanayo na masuala ya kijiolojia kama vile matetemeko, maporomoko ya ardhi na kemikali na madini hatarishi ndani ya udongo na miamba.

Taarifa na tafiti mbalimbali zinazotolewa na GST ni muhimu pia kwa ajili ya kupanga matumizi sahihi na endelevu ya rasilimali ardhi (Land-use planning), ikiwa ni pamoja na utengaji wa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambao kwa sasa wanapewa kipaumbele ili kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika uchimbaji na biashara endelevu ya madini.

Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019, GST imetekeleza miradi mbalimbali ambayo baadhi yake ilifadhiliwa na Serikali na michache ilifadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Baadhi ya kazi hizo zimehusisha ugani wa Jiolojia na Jiokemia katika baadhi ya maeneo katika wilaya za Maswa,Ulanga,Mahenge,Kisarawe, Morogoro Vijijini na Mlandizi.

Aidha taarifa za kijiolojia, jiokemia na ramani zilizozalishwa na taasisi hiyo, zimeweza kusaidia kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira pamoja na kuwa na mipango endelevu ya kilimo na mipango miji.

Kwa mujibu wa Kaimu Mtendaji Mkuu, taasisi hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), wamekamilisha utafiti wa kina wa jiosayansi chini ya mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) uliohusisha jiolojia, jiokemia na jiofizikia kwa lengo la kubaini uwepo na kiasi cha madini kinachopatikana katika maeneo sita ya wachimbaji wadogo.

Maeneo hayo ni Kapanda, D-Reef na Ibindi wilayani Mpanda, Buhemba wilayani Musoma; Katente, Kerezia na Ng'anzo wilayani Bukombe; Itumbi, Mapogolo na Sangambi wilayani Chunya; Kyerwa, Bukoba, Kiomoni, Mkulumuzi na Kange mkoani Tanga.

"Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwepo kwa takribani jumla ya wakia 114,464.65 za dhahabu kwa maeneo ya Katente, Buhemba (Rwabasi), Mpanda (D-Reef and Kapanda) na Itumbi; tani 403,056,469 za limestone zenye ubora wa 48% katika maeneo ya Kiomoni na Mukurumuzi (Tanga) na jumla ya tani 1,409,742.15 za bati katika Wilaya ya Kyerwa," amesema Bibi. Myumbilwa.

Akieleza manufaa ya tafiti hizo, Bibi. Myumbilwa anatanabaisha kwamba matokeo ya utafiti huo, yatawasaidia wachimbaji wadogo kuchimba kwa uhakika na hivyo kuongeza mapato yao na pato la Taifa kwa ujumla.

Akielezea mafanikio mengine ya taasisi hiyo, Myumbilwa amesema kupitia mradi wa SMMRP, taasisi yake ilipata vifaa vya kisasa vya maabara na vya ugani.

Vifaa hivyo ni pamoja na ICP, XRF, AAS with graphite furnace na kuongeza kuwa upatikanaji wa vifaa hivyo utarahisisha utoaji wa huduma za maabara na hatimaye kuongeza ufanisi katika utafiti wa miamba na madini kwa ujumla.



Bibi. Myumbilwa anasema kuwa kwa kutumia fedha za Serikali na kushirikiana na wadau wa maendeleo wameweza kuandaa ramani mbalimbali zinazoonyesha uwepo wa madini kama dhahabu, shaba, chuma, nikeli na bati.

Aidha, GST kwa kushirikiana na Geological Survey of Finland (GTK) ilifanya utafiti wa viwango vya Tindikali na Alkali (Acidity and Alkalinity) kwenye udongo. Viwango hivi vinatofautiana mahala na mahala na taarifa hiyo inaweza kutumika kupanga matumizi sahihi ya udongo kwa kilimo na namna ya kuboresha hali hiyo kwa kutumia madini na kemikali nyingine. Kwa muktadha huo, GST kwa kushirikiana na GTK wanaandaa mpango kazi wa kuboresha viwango vya tindikali na alkali kwenye udongo kwa kutumia miamba. Pia, GST na GTK wamepanga kufanya utafiti wa madini yanayofaa kurekebisha udongo ulioathirika (High acidic and high alkalinity) kwa lengo la kuboresha udongo ili kuongeza uzalishaji wa mazao kwa maeneo tajwa.

Aidha, ili kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji, GST imekamilisha utafiti wa jiosayansi (jiolojia, jiokemia na jiofizikia) katika mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo ramani na taarifa za kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini katika wilaya za Nachingwea na Masasi. Akielezea masuala ya utafiti wa Jiokemia, Kaimu Mtendaji Mkuu huyo anaongeza kuwa GST, kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya China, imekamilisha utafiti wa kina wa jiokemia katika mkoa wa Mbeya na tafiti za awali kwenye maeneo mengine nchi nzima. Aidha, anasema kupitia ushirikiano huo, Atlasi ya Jiokemia ya nchi nzima ilichapishwa na kuongeza kuwa, utafiti huo unatarajiwa kuleta manufaa kwa Taifa hususan katika kujua aina za madini yaliyopo na kwenye miamba na aina ya madini yalizopo kwenye udongo kwa ajili ya kilimo, mazingira na mipango miji.

Vilevile, anasema kuwa, Serikali kupitia GST na kwa ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia National Geographic Information Institute (NGII) imekamilisha tafiti za jiosayansi katika sehemu za maeneo ya Namtumbo, Momba na Tunduru, pia utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege unaendelea katika wilaya hizo ili kukusanya taarifa zitakazosaidi katika katangaza uwekezaji. Katika kuhakikisha kuwa, wachimbaji wanachimba kwa uhakika bila kubahatisha, GST imedhamiria kuhakikisha inafanya utafiti katika maeneo yote nchini na kutoa takwimu sahihi za utafiti kwa wachimbaji ili kuleta tija katika sekta ya madini nchini.

Taasisi ya GST imeanzishwa kutokana na Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2017,  ikiwa na jukumu la kufanya utafiti kuhusu miamba na madini kwa lengo la kutambua viashiria vya madini kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini.






# SOKO LA DHAHABU GEITA

*Soko la Madini lililopo Halmashauri ya Mji wa Geita, Barabara ya Ibanda - Bwanga Mkoani Geita.*





*Uzinduzi wa Soko la Madini Mkoani Geita.*
*Pichani ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, chini kushoto ni Waziri wa Madini Mhe. Doto Biteko (Mb) pamoja na Katibu Mkuu wa Madini Prof. Simon Msanjila.*







# STAMICO YAONGEZA UFANISI KUSAIDIA SEKTA YA MADINI

Na **Mwandishi Wetu**,
Idara ya Habari - **MAELEZO**

Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwekeza kwenye uchimbaji na utafutaji madini, uchenjuaji, kutoa huduma za uchorongaji na ushauri wa kijiolojia ili kushiriki kikamilifu katika kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2015.

Shirika pia limejikita katika uchimbaji madini, kuhamasisha na kuwezesha mabadiliko ya uchimbaji mdogo kuelekea kwenye uchimbaji wa kati ulio rasmi, wenye tija na kulinda mazingira.

Akizunguzia mafanikio ya Shirika hilo, Mtendaji Mkuu wa STAMICO, Kanali Sylvester Ghuliku anaeleza kuwa Serikali ya Awamu ya Tano katika uboreshaji wa mikataba ya ubia wameendelea kunufaika na hatua zinazochukuliwa kati ya Shirika (kwa niaba ya Serikali) na kampuni binafsi katika kuendeleza miradi mbalimbali ya madini.

Kanali Ghuliku anasema katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili, 2017 hadi Machi 2019, Shirika limechimba tani 25,285.50 za makaa ya mawe katika mgodi wa Kabulo ambao ni sehemu ya Mgodi wa Kiwira.

"Hatua hii inalenga kuimarisha ukuaji wa viwanda vya ndani hususan viwanda vya saruji ambavyo ndio watumiaji wakubwa wa madini ya makaa ya mawe na tumeuza tani 1,0891.8 za makaa ya mawe yenye thamani ya shilingi 527,163,120 kwa watumiaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi," anasema Kanali Ghuliku.

Akizungumzia kuhusu uuzaji wa madini ya dhahabu na fedha, Kanali Ghuliku anasema Shirika limesimamia uzalishaji na uuzaji wa madini ya dhahabu na madini ya fedha kutoka katika mgodi wake wa STAMIGOLD uliopo wilayani Biharamulo mkoani Kagera.

Mgodi wa STAMIGOLD ni Kampuni Tanzu ya STAMICO iliyoanzishwa Mwaka 2013. Awali, ulijulikana kama mgodi wa Tulawaka chini ya umiliki wa kampuni ya African Gold Barrick. Mgodi unaendeshwa na Watanzania kwa asilimia 100 na umetoa ajira kwa wafanyakazi 225 walioajiriwa moja kwa moja na mgodi na wafanyakazi wa wazabuni zaidi ya 250.

Anaongeza kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2014 hadi kufikia mwezi Machi, 2019, mgodi huo umezalisha na kuuza jumla ya wakia 68,762.37 za madini ya dhahabu na wakia 7,928.97 za madini ya fedha, huku kipindi cha Oktoba 2015 hadi Machi 2019, mgodi umeuza madini ya dhahabu na fedha yenye thamani ya Dola za Marekani 75,638,607.78.

Ikiwa ni moja ya majukumu yake ya kutekeleza shughuli za uchimbaji katika sekta ya madini, STAMICO imeendelea na usimamizi wa mgodi wa TanzaniteOne uliopo wilayani Simanjiro mkoani Manyara ambao umezalishaji na uuzaji wa madini ya jumla ya Kilo 12,452.86 za Tanzanite yenye thamani ya shilingi bilioni 60.48 kati ya Oktoba 2015 hadi Disemba 2017 uzalishaji uliposimama. "Sanjari na hilo, Serikali inaendelea kuboresha Mkataba wa Ubia kati yake na kampuni ya Tanzanite One Mining Limited ili kuongeza ushiriki na manufaa ya Serikali kutokana na uendeshaji wa mradi huo," anasema Kanali Ghuliku.

"Kama nilivyoeleza awali, moja ya majukumu ya STAMICO ni kuhamasisha na kuwezesha mabadiliko ya uchimbaji mdogo kuelekea kwenye uchimbaji wa kati ulio rasmi, kwa kutambua umuhimu wa wachimbaji wadogo hapa nchini, STAMICO ilianzisha mradi wa ununuzi wa madini ya bati kutoka kwa wachimbaji wadogo wa maeneo ya Kyerwa Syndicate, Murongo, Kabingo na Rugasha mkoani Kagera kwa lengo la kuwapatia soko imara wachimbaji wa madini hayo. "Kuanzia katikati ya Mwaka 2016 ambapo mradi huo ulianza hadi kufikia Julai, 2017 jumla ya tani 106.27 za madini hayo yenye thamani ya Shilingi 1,570,996,000 yalinunuliwa kutoka kwa wachimbaji wadogo," alisema ingawa kwa sasa ununuzi huo umesimama.

Mbali na hayo, STAMICO inasimamia miradi ambayo inachangia katika Mfuko wa Taifa kwa kulipa Mrabaha na Ushuru wa Huduma kadri inavyoelekezwa katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017. Hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Shirika kupitia miradi yake ya Kabulo (Makaa ya Mawe) STAMIGOLD (Dhahabu na Fedha), Kyerwa (Tin) na TanzaniteOne (Tanzanite), limelipa mrabaha wa shilingi bilioni 10.92.

Vilevile, mbali na uchimbaji, huduma nyingine zinazotolewa na Shirika hilo ni kutoa huduma za kibiashara za uchorongaji na ushauri wa kitaalam wa kijiolojia na kihandisi ambapo katika pindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Machi, 2019 Shirika limekamilisha uchorongaji wa mita 2,434 wa aina ya Diamond (DD) na mita 8,200 za aina ya Reverse Circulation (RC) pamoja na utoaji wa kandarasi tano za ushauri wa kijiolojia.

Akizungumzia umuhimu wa jamii zinazoizunguka migodi yake, Kanali Ghuliku anasema Shirika limeendelea kuchangia ukuaji wa huduma mbalimbali za kijamii katika nyanja za elimu, afya, barabara, mazingira pamoja na ulinzi na usalama. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Shirika limechangia shilingi bilioni 1.85 katika uendelezaji wa shughuli hizo kupitia miradi ya STAMIGOLD ya Buhemba na Tanzanite One. Kuhusu shughuli za utafiti, anasema kupitia mgodi wa STAMIGOLD, Shirika limeendelea kufanya utafiti wa dhahabu ikiwa ni pamoja na uchorongaji.

"Utafiti huu umezaa matokeo chanya ambapo kampuni imeweza kubaini uwepo wa mbale tani 1,132,548 zenye grade ya 1.12g/t ambazo zina takribani jumla ya wakia 40,649 za dhahabu katika maeneo ya pit 03, pit 04, project 08 na West pit extension gap," anasisitiza Kanali Ghuliku.

Akifafanua zaidi kuhusu taarifa za utafiti, anasema Shirika limekamilisha uhakiki wa mashapo ya dhahabu katika mashimo manne kati ya sita ya mradi wa Buhemba. Katika uhakiki huo, wakia 441,772 za mashapo ya dhahabu (indicated resources) zimethibitika kuwemo katika mashimo hayo ya Buhemba 1, Buhemba 4,Kilamongo South na Kilamongo North.

Anaongeza kwamba, Shirika linatarajia mashapo ya mradi huo yataongezeka na kufikia zaidi ya wakia 600,000 mara uthibitishaji utakapokamilika katika mashimo mawili ya Mwizi na Buhemba Main.

Mbali na hilo, Shirika limekamilisha utafiti wa kina wa kijiosayansi na kuwasilisvJiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), limetoa mafunzo juu ya taarifa za kijiolojia na mashapo ya madini kwa wachimbaji wadogo takribani 600 katika maeneo ya uchimbaji mdogo ya Katente, Kyerwa, Itumbi, Buhemba, Mpanda na Tanga. Mafunzo haya yalifanyika kwa kushirikiana GST

"Taarifa hizi zitawawezesha wachimbaji wadogo kuweka mipango sahihi ya uchimbaji katika maeneo yao kwa kujua aina ya vifaa vya uchimbaji vinavyohitajika na aina ya miamba yenye madini," anasema Ghuliku. Aidha, katika jukumu lake la kutoa huduma za uchorongaji, Wizara kupitia mradi wa SMMRP ilinunua mtambo kwa ajili ya shughuli za uchorongaji na kukabidhiwa kwa STAMICO kwa ajili ya uendelezaji wa uchimbaji mdogo na wa kati nchini.

Kutokana na mafanikio hayo, hivi karibuni wakati wa vikao vya Kamati, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ilipongeza juhudi zinazofanywa na Shirika hilo kutokana na mafankio yaliyopatikana katika kuendeleza mgodi wake wa Kiwira, kuendeleza shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe kupitia mgodi wake wa Kabulo na uzalishaji katika mgodi wa STAMIGOLD.

Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) lilianzishwa mwaka 1972, na baadae kufanyiwa Maboresho Machi 5, Mwaka 2015 kwa lengo la kuifanya STAMICO kushiriki na kusimamia maslahi ya Serikali na kuwekeza kimkakati katika Sekta ya madini kama yalivyoainishwa katika Hati ya Kurekebisha Uanzishwaji wa STAMICO (The Public Corporation State Mining Corporation Establishment Amendment Order, 2015).



# CHUO CHA MADINI CHACHU YA KUIONGEZEA SEKTA THAMANI

Na **Mwandishi wetu**

Katika mageuzi yanayoendelea kwenye sekta ya madini moja ya eneo linaloimarishwa ili kuiongezea thamani sekta hii ni elimu kuhusu mawanda mbalimbali ya kisekta. Miongoni mwa taasisi zilizoimarishwa ili kushabihisha uchumi wa viwanda kupitia sekta ya madini, ni Chuo cha Madini (MRI) kilichopo Dodoma ambacho kimepata mafanikio makubwa katika nyanja za utoaji mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali.

Miongoni mwa fani zinazotolewa katika Chuo cha Madini ni: Jiolojia na Utafutaji Madini, Uhandisi Migodi, Uhandisi Uchenjuaji Madini, Sayansi ya Mafuta na Gesi, Uhandisi Mazingira, Usimamizi Migodini pamoja na Upimaji Ardhi na Migodi.

Mafanikio ya Chuo hiki yanatokana na hamasa iliyojengeka katika sekta ya madini na hivyo kupata fursa ya kuwasaidia Watanzania wengi kupata elimu na uelewa mpana juu ya rasilimali madini.



*Wanafunzi wa Chuo cha Madini Dodoma (MRI) wakiwa katika mafunzo kwa vitendo.*



## UHUSISHAJI WA CHUO

Kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Madini, Fredrick Mangasini amelieleza Jarida la Nchi Yetu kuwa katika kuongeza wigo wa kutoa elimu bora na nafuu pamoja na kusogeza huduma kwa Watanzania, Chuo kimesajili na kuanzisha mafunzo katika kampasi mpya wilayani Nzega mkoani Tabora katika eneo lililokuwa linamilikiwa na kampuni ya uchimbaji madini ya Resolute (Tanzania) Ltd.

Mkuu wa Chuo amesema uanzishwaji wa kampasi ya Tabora ambayo imeshapatiwa usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTE), kutasaidia kupata wataalamu wanaotambulika kitaifa na hata kimataifa katika kuinua sekta ya madini.

Katika kuhakikisha kwamba wataalam wa madini wanaongezeka nchini, Kampasi ya Tabora imeendelea kupata idadi kubwa ya wanafunzi ambapo imedahili wanafunzi 97 kufanya mafunzo ya muda mrefu ambapo wanaume ni 83 na wanawake ni 14.

Mbali na kuanzishwa kwa kampasi hiyo, vile vile Chuo kwa Kampasi Kuu ya Dodoma, kimeongeza udahili kutoka wanafunzi 245 mwaka 2013/2014 hadi kufikia wanafunzi 604 mwaka 2018/2019.

Huu ni mwelekeo kuwa katika miaka michache ijayo wataalam wa madini wataongezeka na hivyo kusaidia ukuaji wa sekta.



*Wanafunzi wa Chuo cha Madini Dodoma wakiwa katika mafunzo kwa vitendo.*

## MAFUNZO KWA WACHIMBAJI WADOGO

Kwa kutambua mchango wa wachimbaji wadogo kwenye sekta ya madini na katika Pato la Taifa, Chuo kimeendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuanzisha mafunzo maalum kwa wachimbaji wadogo.

Hadi kufikia Disemba, 2018, wachimbaji wadogo wapatao 117 walipewa mafunzo kwenye maeneo ya utafutaji na uchimbaji madini, uchenjuaji madini, afya na usalama mahali pa kazi, pamoja na utunzaji wa mazingira.

Aidha, Bw. Mangasini anaeleza kuwa Chuo kimeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wachimbaji wadogo na kwamba kimefanikiwa kuanzisha kozi mpya ya Upimaji Ardhi na Migodi katika ngazi ya Cheti na Stashahada.

Anasema kozi hiyo imeanzishwa ili kuzalisha wataalam wazawa watakaofanya upimaji wa ardhi migodini na pia wataalam hao watasaidia kutatua migogoro ya ardhi migodini hususani tatizo la muda mrefu la mitobozano (wachimbaji kuchimba madini hadi kukutana chini ya ardhi) katika machimbo ya vito na madini ya metali kutokana na kutokuwepo mipaka inayojulikana.

Pamoja na kazi kubwa iliyofanyika katika kupanua wigo wa utoaji mafunzo kwa wataalam pamoja na wachimbaji wadogo, miundombinu ya chuo imeendelea kuimarishwa ili kuongeza wataalam zaidi.

Wizara ya Madini kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP), inajenga jengo la taaluma katika Kampasi ya Dodoma litakalokuwa na ofisi 50 za wakufunzi, vyumba viwili vya mihadhara, chumba kimoja cha mikutano pamoja na chumba kimoja cha kuhifadhia mitihani.


Ni dhahiri kwamba kwa juhudi za sasa za Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha Taifa linafaidika na sekta ya madini, uboreshaji na uhuishaji wa Chuo hiki utakuwa ni chachu nyingine muhimu katika kuiongezea sekta thamani.

**TEITI** Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative

Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

# MFUMO WA KIELETRONIKI KWA AJILI YA KUWEKA TAKWIMU ZA TEITI KWENYE VIELELEZO (DASHBOARDS) SASA UPO WAZI KWA AJILI YA WANANCHI KUTEMBELEA KUPITIA TOVUTI YETU

www.dashboard.teiti.go.tz




**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**S.L.P. 422,**
**40474,**
**DODOMA, TANZANIA**

**Kwa Mawasiliano**
**info@teiti.or.tz**




# TEITI YAIMARISHA UWAZI, UWAJIBIKAJI SEKTA YA MADINI

Na **Mwandishi** Wetu

Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (TEITI), imeendelea kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika sekta za madini, mafuta na gesi asilia kwa kutoa ripoti kwa wananchi na viongozi wa Serikali juu ya uwazi na uwajibikaji katika kampuni zinazochimba rasilimali za asili nchini Tanzania.

Kaimu Katibu Mtendaji wa TEITI, Mariam Mgaya amelieleza Jarida la Nchi Yetu kuwa katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji, Taasisi inaangalia maeneo kadhaa yakiwemo utoaji wa leseni na mikataba ya uchimbaji madini, mafuta na gesi asilia, ukusanyaji mapato na mgawanyo wa mapato na matumizi ili nchi iweze kunufaika narasilimalihizo.

Ameeleza kuwa katika kusimamia uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini, mafuta na gesi asilia, TEITI imefanikiwa kutoa ripoti nane kwa vipindi vya Miaka ya Fedha 2008/09 hadi 2015/16, ambapo ripoti hizo zinaonesha kuwa Serikali imepokea kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.96 ikiwa ni kodi mbalimbali zilizolipwa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zilizofanyiwa ulinganisho.

Anaeleza zaidi kuwa elimu juu ya matumizi ya takwimu zilizopo katika ripoti za TEITI imetolewa na kusaidia viongozi wa vijiji wakiwemo Madiwani, kuwahoji viongozi wao katika halmashauri au Maafisa wa Serikali kwa kutumia takwimu zilizohakikiwa kutoka kampuni na Serikalini.

Anatolea mfano wa Halmashauri za Geita, Kahama, Mtwara na Kilwa kama ni miongoni mwa halmashauri zilizotumia ripoti za TEITI na kusaidia watumishi wa halmashauri kuhakiki na kulinganisha malipo mbalimbali ya tozo zilizotolewa kwa kukokotoa kutoka katika takwimu za uzalishaji kwa mwaka ambapo wananchi pia wanapata fursa ya kujua.

"Katika haya yote niseme kumekuwepo na kuongezeka kwa uwazi juu ya matumizi ya mapato ya halmashauri yanayotokana na tozo kutoka kampuni za uchimbaji wa Madini, Mafuta na Gesi Asilia," anaongeza Mgaya.





Akifafanua zaidi kuhusu namna Tanzania inavyotekeleza mfumo wa TEITI, anasema Januari, 2017 Tanzania ilifanyiwa tathmini ya pili na Taasisi ya Kimataifa ya The Extractive Transparency Initiative (EITI) juu ya utekelezaji wa vigezo vya uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

Kufuatia tathmini hiyo mwezi Oktoba 2017, Tanzania ilitunukiwa hadhi ya "Meaningful Progress" kwa maana ya kwamba nchi inapiga hatua muhimu katika masuala ya uwazi na uwajibikaji ikilinganishwa na tathmini ya kwanza ambapo nchi ilitunukiwa hadhi ya "Compliant" kwa maana ya kuwa imekidhi tu vigezo.

Naye Mwenyekiti wa TEITI, Bw.Ludovick Utouh anasema taasisi hiyo pia ina jukumu la kuhakikisha kampuni zinayofanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, mafuta na gesi asilia zinaweka wazi taarifa za shughuli zao kulingana na Sheria ya TEITA ya mwaka 2015.

Anasema kuwa ni muhimu kwa wadau kuwa na uelewa wa kutosha ili kuwawezesha kuwajibika kulingana na Sheria za nchi na viwango vya kimataifa na kuongeza kuwa katika kuhakikisha kwamba taarifa kuhusu rasilimali hizo zinapatikana kwa uwazi, tayari TEITI imezindua mfumo wa kuwawezesha wadau kupata taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya sekta za madini kupitia:
**www.dashboard.teiti.go.tz.**

Akizungumza hivi karibuni wakati wa mkutano wa wadau wa sekta za madini, mafuta na gesi asilia, Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko amezitaka kampuni zilizowekeza katika sekta ya madini nchini, kushirikiana na TEITI kutoa taarifa sahihi na kwa wakati juu ya uwekezaji wao huku akiwataka wamiliki wa migodi kuwa na mahusino mazuri na wananchi wanaozunguka migodi ili kujihakikishia ulinzi, usalama na amani.


Aidha, ili kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji katika masuala ya madini nchini, amewataka wawekezaji kuweka kumbukumbu zao vizuri ili pindi zinapohitajika zipatikane kwa urahisi na hivyo kupunguza au kutokomeza kabisa rushwa na urasimu nchini.

TEITI ilianzishwa chini ya Sheria Na. 23 ya Mwaka 2015 (The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability-TEITA)-Act, 2015) kwa lengo la kusimamia shughuli za uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia Tanzania.



# MBEYA WATEKELEZA AGIZO LA RAIS SOKO LA DHAHABU CHUNYA

*Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila akizungumza katika Uzinduzi wa Soko la Dhahabu Chunya, Mkoani Mbeya.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof.Simon Msanjila (kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mary-Prisca Mahundi na Mwisho Kulia ni Mwenyeketi wa Tume ya Madini Prof. Idris Kikula wakishiriki uzinduzi wa Soko la Madini Chunya, Mei, 2019.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Madini Prof. Simon Msanjila (kushoto) akipeana mkono na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mary-Prisca Mahundi wakati wa Uzinduzi wa Soko la Madini Wilayani Chunya, Mkoani Mbeya, Mei, 2019.*



# TGC CHACHU KUFIKIA LENGO KUYAONGEZEA THAMANI MADINI

Na **Mwandishi Maalum**

Kituo cha Jemolojia (TGC) kilianzishwa mwaka 2003 kikijulikana kama Arusha Gemstone Carving Centre (AGCC), ikiwa wakati huo Serikali inatekeleza Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Madini (Mineral Sector Development Technical Assistance - MSDTA) uliotekelezwa Kati mwaka 1994 na 2005 kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Wakati huo, lengo la kuanzisha Kituo lilikuwa ni kutekeleza Sera ya Madini ya Mwaka 1997 kuhusu uongezaji thamani madini nchini kwa kujihusisha na uchongaji wa vinyago vya miamba (Stone Carving) na utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo.

Hadi kufikia mwaka 2018, Kituo kilikuwa kimetoa wahitimu 103.

Akizungumza wakati wa ziara yake kituoni hapo, Naibu Waziri wa Madini, Mhe. Stanslaus Nyongo alisema, Serikali imeanza kufanya taratibu za kupeleka maombi ya kuondoa kodi ya vifaa vya uongezaji thamani madini kwa Mamlaka husika ili kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya uongezaji thamani madini nchini ikiwemo kupanua wigo wa ajira na kuongeza mapato kupitia sekta ya madini.

Aidha, katika jitihada za kukifanya kituo cha TGC kijiendeshe kibiashara katika tasnia ya uongezaji thamani madini nchini, kupitia mradi wa SMMRP, wizara imeandaa Mpango wa Kibiashara na Mpango Mkakati wa kituo hicho ili kukiimarisha kwa lengo la kuzalisha wataalam katika tasnia hiyo ambayo hivi sasa suala la uongezaji thamani katika madini limepewa kipaumbele.

Wakati duniani kote madini yanakuwa na bei nzuri baada ya kuongezewa thamani, Serikali ya Tanzania kupitia Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) cha jijini Arusha imeona umuhimu huo na kuanza kujikita katika kutoa mafunzo ya kuongeza thamani ya madini ili kuongeza mchango wa sekta hiyo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa.

Akieleza maendeleo ya Kituo hicho muhimu kwa nchi, Kaimu Mratibu wa TGC, Bw. Erick Mpesa, anaeleza kuwa kwa sasa Kituo hicho kinatoa mafunzo ya Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) ikiwa ni jitihada za kusaidia juhudi za Serikali za kuhakikisha madini yote yanayozalishwa nchini yanaongezwa thamani kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

“Nchi hii imebarikiwa kuwa na madini ya kila aina na kwa sasa Serikali imeweka mkakati wa kuongeza thamani madini yanayozalishwa nchini.
Jukumu letu katika Kituo hiki ni kuhakikisha tunatoa wataalam wengi watakaotumika katika kuongeza thamani ya madini ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi,” anaeleza Mpesa.

Mpesa anasema dhima ya Kituo hicho ni kutoa huduma bora za kijimolojia katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki na Kati, kwa kutoa mafunzo na uhamasishaji wa uongezaji thamani wa Madini yaVito na mawe ya mapambo.

Katika kuhakikisha TGC kinakuwa kituo bora katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Wizara ya Madini kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) umekijengea uwezo kituo hicho kwa kufanya ukarabati wa majengo na kununua thamani na vifaa vya kufundishia katika fani za ukataji na unga’arishaji vito na usonara.

Kupitia Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Serikali iliazimia kuongeza manufaa yatokanayo na sekta ya madini na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini kufanyika hapa nchini.

Ili kutekeleza hilo, shughuli za Kituo zilipanuliwa na kulazimu kufanya ukarabati ili kuhimili mahitaji halisi ya sasa ya kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito katika fani za ukataji na ung’arishaji madini ya vito (lapidary), utambuzi wa madini ya vito (Gemology) na usonara (Jewelry design & Manufacturing).

Aidha, katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha madini yanaongezewa thamani nchini, Wizara ilipeleka watumishi watatu nje ya nchi ili kupata mafunzo ya Ukufunzi katika fani za jimolojia, ukataji na ung’arishaji madini na usonara. Mpesa anaeleza kuwa katika kupanua wigo wa shughuli za uongezaji thamani madini, Januari mwaka huu, kituo kimeanza kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utambuzi wa Madini ya Vito na Usonara.




*Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt.John Pombe Magufuli akizungumza katika mkutano wa wadau wa Madini Tanzania uliofanyika mwezi Januari 2019, Kushoto kwake ni Waziri wa Madini, Mhe.Doto Biteko.*

# MKUTANO WA WADAU WA MADINI, JANUARI 22, 2019





*Waziri wa Madini Mhe. Doto Biteko (Mb) akizungumza kwenye Mkutano wa Wadau wa Madini Tanzania uliofanyika mwezi Januari, 2019. Kulia kwake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli. Kushoto kwake wa kwanza ni Rais wa FEMATA Bw. John Bina akifuatiwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul Makonda.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akipokea ripoti ya Maazimio ya Mkutano wa Wadau wa Madini Tanzania uliofanyika mwezi Januari, 2019.*



# MGODI WA BUSOLWA: TUNANUFAIKA NA MAGEUZI YA JPM

Na **Mwandishi wetu**

MGODI wa Busolwa ni mfano hai wa namna Watanzania wanavyoshiriki na kunufaika na rasilimali zao za madini kwa kushiriki katika uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini kwa ujumla.

Kampuni ya Busolwa Mining Limited ni miongoni mwa kampuni za wazawa ambayo inashiriki kikamilifu katika uchimbaji wa madini ya dhahabu na kuwanufaisha watanzania kupitia fursa mbalimbali zikiwemo ajira.

Kampuni hii pia ni miongoni mwa wanufaika wa mageuzi mbalimbali yanayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kampuni hii inayomilikiwa na Mtanzania, Bw. Baraka Ezekiel Nyandu, ilisajiliwa mwaka 2014 kufanya shughuli za uchimbaji dhahabu katika eneo lenye kilomita za mraba 0.53 katika kijiji cha Busolwa, Kata ya Nyarugusu, wilayani Geita.

### Mchango Katika Uchumi

Akizungumza na Jarida la Nchi Yetu kueleza safari yake ya kufanikisha uwekezaji huo, Bw. Nyandu, anaeleza kuwa tangu mgodi huo uanze kazi rasmi za uchimbaji madini mwezi Septemba 2015, kumekuwa na mafanikio makubwa ambapo mpaka sasa mgodi umetoa ajira za moja kwa moja kwa watanzania zaidi ya 295 na ajira 60 zisizo za moja kwa moja.

"Mafanikio haya yanatokana na uwekezaji wa Dola za Kimarekani milioni 25 tulioufanya na pia juhudi zinazofanywa na Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ikiwemo kuwawezesha na kuwahamasisha wazawa katika sekta ya madini," anaeleza Bw. Nyandu.

Anaongeza kuwa mafanikio mengine ni pamoja na kampuni hiyo kushiriki katika shughuli za maendeleo katika Mkoa wa Geita ikiwemo kuchangia madawati 2,600 kwa ajili ya shule mbalimbali, ujenzi wa choo katika shule ya Msingi Tologo, ukarabati wa bwawa la Nyasale, ukarabati wa barabara yenye urefu wa kilometa 36 na ujenzi wa ofisi ya Serikali ya Kijiji cha Buswelu.

Kwa mujibu wa Nyandu, mbali na kushiriki shughuli za maendeleo, mgodi huo unalipa kodi zote za Serikali ikiwemo mrahaba ambapo katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017 wamelipa jumla ya shilingi 1,016,574,487 (kodi mbalimbali za mapato na mrahaba), shilingi milioni 340 kodi ya mapato na shilingi milioni 68.4 kodi ya zuio.

Anafafanua zaidi kuwa kampuni hiyo pia imekuwa ikishirikiana na Serikali katika matukio ya uokoaji wachimbaji wadogo wanaofukiwa na migodi kwa kutoa vifaa na wataalamu wa uokoaji.

### Shukrani kwa Serikali

Bw. Nyandu ameishukuru Serikali kwa mambo mengi ya kisera na kisheria ikiwemo hamasa ya kuisaidia sekta ya madini.

Kikubwa anataja kupigwa marufuku usafirishaji wa madini ghafi ikiwa ni pamoja na mchanga wenye madini (minerals concentrates) kabla ya kuongeza thamani.

Anakiri zuio hilo limewezesha kuanzishwa kwa viwanda vya uchenjuaji madini na hatimaye kuongezeka kwa mapato yatokanayo na Sekta ya madini pamoja na kuongezeka kwa ajira hapa nchini.

Anasema pia zuio la kusafirisha kaboni zenye dhahabu kusafirishwa nje ya mkoa limeongeza fursa ya uwekezaji ambapo kampuni hiyo imefunga mtambo wa kisasa wa kuchenjua dhahabu (Elusion Plant) wenye uwezo wa kuchakata hadi tani 1,200 za kaboni kwa siku.

Kwa mujibu wa Nyandu, uhai wa mgodi wa Busolwa Mining Limited ni miaka kumi kwa uchimbaji wa wazi (Open Pit) ambapo kwa kipindi hicho, mgodi huo unatarajia kuzalisha wastani wa wakia 200,000 sawa na takribani tani 5.7 za dhahabu.

Kwa sasa uzalishaji wa dhahabu nchini unakadiriwa kuwa kati ya tani 48 mpaka 50 kwa mwaka. Kukua kwa Mgodi huu na mafanikio unayoendelea kuyapata ni ishara kuwa sera nyingi zinazotekelezwa na Rais Magufuli na Serikali kwa ujumla zina manufaa makubwa kwa Tanzania ya sasa na ijayo.




SUPER RAMP
52728




# UDHIBITI SEKTA YA MADINI
## WAONGEZA UZALISHAJI MWADUI

**Na Mwandishi Maalum, Mwadui**

Uthibidi na usimamizi makini wa Sheria katika sekta ya madini umeonesha mafanikio ambapo Mgodi wa Williamson Diamond Limited (WDL) maarufu kama Mwadui, umefanikiwa kuzalisha madini ya almasi karati 1,154,753.44 katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2018, kutoka karati 486,561.68 zilizozalishwa kati ya mwaka 2012 hadi 2014.

Karati hizo 1,154,753.44 zilizozalishwa kati ya 2015 hadi 2018, ni sawa na wastani wa karati 288,688.36 kwa mwaka, ikiwa ni ongezeko la karati 126,501.13, sawa na ongezeko la asilimia 44 ukilinganisha na kipindi kati ya mwaka 2012 hadi 2014.

Madini ya almasi yaliyozalishwa katika kipindi hicho yalikuwa na thamani ya dola za Marekani 329,332,364.32 ambazo ni sawa na wastani wa dola za Marekani 82,333,091.08 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Meneja Ukaguzi wa Uzalishaji na Biashara wa Tume ya Madini,

George Kaseza, thamani ya madini haya kati ya mwaka 2015 – 2018 imeongezeka kwa wastani wa dola za Marekani 35,588,623.08, ikilinganishwa na kipindi cha kati ya mwaka 2012 hadi 2014 ambapo thamani ya madini yaliyozalishwa ilikuwa ni dola za Marekani 140,233,404 ambayo ni wastani wa dola za Marekani 46,744,468 kwa mwaka.

"Ongezeko hili kubwa la madini ya almasi limetokana na kuongezeka kwa usimamizi na udhibiti katika hatua zote kuanzia uzalishaji, uthaminishaji na kwenye minada ya almasi nje ya nchi," anaeleza Kaseza.

Anasema mapinduzi hayo makubwa katika sekta ya madini yanatokana na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ya kuhakikisha kuwa watanzania na Taifa kwa ujumla wanafaidika na rasilimali madini.

Mwaka 2017 Bunge lilifanya marekebisho makubwa katika Sheria ya Madini,2010 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 7 ya mwaka 2017.

Mabadiliko hayo yaliweka uthibiti zaidi wa sekta ya madini nchini na kuiweka rasilimali madini mikononi mwa Rais kama msimamizim kwa niaba ya wananchi.

Mgodi wa Almasi wa Williamson Diamond Limited ulifunguliwa miaka ya 1940 katika eneo la Mwadui mkoani Shinyanga. Mgodi huu ulikuwa moja ya migodi mikubwa sana Duniani na uliifanya Tanzania kuwa miongozi mwa nchi zenye shughuli kubwa za uchimbaji madini.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt.John Pombe Magufuli katika picha ya pamoja na Mawaziri, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu baada ya uzinduzi wa Ukuta unaozunguka Migodi ya Tanzanite Mirerani,Wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara.*

# UZINDUZI WA UKUTA WA MAGUFULI
# MIRERANI, APRILI 6, 2018



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt.John Pombe Magufuli akizungumza jambo na Mgunduzi wa Madini ya Tanzanite, Marehemu Jumanne Mhero Ngoma. Mwisho kulia ni Mke wa Rais Mama Janeth Magufuli wakati wa hafla ya uzinduzi wa Ukuta unaozunguka Migodi ya Tanzanite Mirerani, Wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara.*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akipeana mkono na Waziri wa Madini Mhe. Doto Biteko baada ya uzinduzi wa Ukuta wa Mirerani.*



*Mawaziri pamoja na Naibu Mawaziri wakiwa katika uzinduzi wa Ukuta wa Mirerani,Wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara.*


DESTINATION TANZANIA
VISIT TANZANIA!
#UnforgettableTanzania


DESTINATION
TANZANIA
#DestinationTanzania
#DestinationTanzania Ukurasa mpya unaoendeshwa na IDARA YA HABARI-MAELEZO kuitangaza Tanzania yetu, Utalii wake, Utamaduni wake, Rasilimali zake, Maendeleo yake na kila zuri lake.
DestinationTanzania

# Nukuu Muhimu...

Tutawafuata kokote tutakaposikia taratibu za uchimbaji na biashara ya madini hazifuatwi

**Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko (Mb)**

" Soko hili la Madini Chunya litaondoa uwezekano wa wanunuzi wa madini kuibiwa na wajanja wachache wanaojifanya kuwa na madini wakati hawana, nawasihi wanunuzi wa madini kuyatumia masoko kikamilifu ili kuepuka udanganyifu na utapeli,"

**Katibu Mkuu Wizara ya Madini,**
**Prof.Simon Msanjila**

Mimi kama Waziri mwenye dhamana katika sekta hii ya Madini ninawapenda sana wachimbaji lakini nasikitika sana kwa wachimbaji na wenye kampuni za uchenjuaji kutokuwa waaminifu

**Waziri wa Madini, Mhe. Doto Biteko (Mb)**

"Hakuna tatizo lolote kwenye Sheria ya Madini. Hata wageni huwa tunakaa nao tunawaelimisha na wanatuelewa vizuri.
Kama kuna dosari za kiutendaji ni vitu ambavyo tunaweza kuvirekebisha na tayari tumekwishakufanya hivyo kwa baadhi ya maeneo,"

**Katibu Mkuu wa Madini,**
**Prof. Simon Msanjila.**

Mchimbaji ambaye anakwepa kulipa kodi mbalimbali kama Sheria ya Madini na Kanuni zake inavyofafanua ni adui namba moja katika ukuaji wa maendeleo ya nchi, hivyo sisi kama Wizara ya Madini tumejipanga kuchukua hatua za kisheria nia ikiwa ni kutaka kila mwananchi anufaike na rasilimali za madini kupitia uboreshaji wa huduma mbalimbali

**Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo**

"Katika kusimamia uchimbaji mdogo, Serikali kupitia Wizara ya Madini inatekeleza mambo kadhaa muhimu pamoja na kuhakikisha wachimbaji wote wanarasimishwa kwa kupatiwa leseni."

**Kamishna wa Madini,**
**Mhandisi David Mulabwa**

Wamiliki wa leseni wanaotumia mrabaha kwa ajili ya kufanya masuala mengine ya kijamii wanakiuka taratibu. Fedha za kufanyia shughuli za maendeleo zinapaswa kutoka katika fedha za Uwajibikaji kwa jamii ambazo Halmashauri zinapanga kupitia Baraza la Madiwani

**Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MADINI
# KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

**MAHALI: Kituo cha**

**Jemolojia Tanzania (TGC), Jijini Arusha**

**MAFUNZO YANAYOTOLEWA**: Shahada katika Teknolojia ya Madini ya Vito na Usonara ( Diploma in Gem and Jewellery), Cheti katika fani za Ukataji, Unga'rishaji madini ya Vito (lapidary), uchongaji wa vinyago na miamba (Gem & Rock Carving), elimu ya sayansi ya madini ya vito (gemology) pamoja na usonara (Jewellrey Design and Jewellery Manufacturing).

PIA: Kituo kinatengeneza bidhaa za uremnbo na mapambo, mikufu, pete, heleni, vikuku kwa kutumia madini na miamba.

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA:**

1. Huduma za kusanifu madini ya vito na miamba.

2. Utambuzi wa madini ya vito, utengenezaji wa bidhaa za mapambo na marembo (usonara).

3 .Kufanya tafiti (research) na kutoa huduma za ushauri na ugani (consultation services) kuhusiana na madini ya vito na usonara.

4. Kutoa huduma za kimaabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara kwa kutoa vyeti vya uthibitisho (certificate of authenticity).

5. Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini.



MAWASILIANO:

**Mratibu,**
**Kituo cha Jemolojia Tanzania**
**S.L.P 119,**
**Arusha**
**Baruapepe: tgc@madini.go.tz**
**Simu: +255 27 254 3241**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA MADINI
CHUO CHA MADINI DODOMA
S. L. P 1696, Dodoma
Simu: +255 26 2300472, Fax: +255262963003
Baruapepe: info@mri.ac.tz/principal@mri.ac.tz/registrar@mri.ac.tz
Tovuti: www.mri.ac.tz
(KIMEPEWA ITHIBATI KAMILI NA NACTE)

# NAFASI ZA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA NGAZI YA ASTASHAHADA/ STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Chuo cha Madini ni Chuo cha Serikali kipo chini ya Wizara ya Madini, kina uzoefu wa zaidi ya miaka thelathini (30) katika kufundisha wataalamu wa ngazi ya kati katika sekta ya madini. Mnamo mwaka 2012, Chuo cha Madini kilianza pia kutoa mafunzo katika sekta za Mafuta, Gesi na Mazingira; na mwaka 2018 Chuo kilianza kutoa mafunzo ya Upimaji Ardhi na Migodi.

Chuo cha Mdini kina ithibati kamili ya Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi *(NACTE)* kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada hadi Stashahada *(NTA level 4 - 6)* katika mfumo wa umahili *(CBET)*.

Chuo cha Madini kinakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa kuomba nafasi za masomo kwa ngazi ya Astashahada/Stashahada kwa kozi zifuatazo:

- **Jiolojia na Utafutaji Madini (Geology and Mineral Exploration)**
- **Uhandisi Migodi (Mining Engineering)**
- **Uhandisi Uchenjuaji Madini (Mineral Processing Engineering)**
- **Sayansi ya Mafuta na Gesi (Petroleum Geosciences )**
- **Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini (Environmental Engineering and Management in Mines)**
- **Upimaji Ardhi na Migodi (Land and Mine Surveying)**

## SIFA ZA KUJIUNGA

- Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne (Form IV) na awe amefaulu masomo ya Fizikia, Kemia, Hisabati na masomo mengine mawili (2) yasiyo ya dini kwa kiwango cha kuanzia D.
- Awe na cheti cha kidato cha nne (Form IV) na kufaulu masomo manne (4) ya sayansi (Kwa waombaji wa kozi ya Upimaji Ardhi na Migodi-***Land and Mine Surveying*** tu)

## NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

***Waombaji wote wenye sifa wanatakiwa kujaza fomu za maombi na kuzituma Chuoni moja kwa moja. Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Madini Kampasi ya Dodoma na Nzega, Ofisi za Wizara ya Madini, Ofisi za Madini zilizopo Mbeya, Tabora, Mwanza, Kahama, Dar es Salaam, Musoma, Songea, Arusha, Tanga, Tunduru, Dodoma, Morogoro, Handeni, Merelani, Mpanda, Bukoba, Mtwara, Shinyanga, Chunya, Moshi, Nachingwea, Geita, Bariadi, Singida na Kigoma, au katika tovuti ya chuo: www.mri.ac.tz***

*Kwa maelezo/msaada zaidi wasiliana nasi kupitia:* ***0784 893 116 / 0764 910 385 / 0712650177 / 0753 858 028***

**Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 30/8/ 2019 saa 9:30 alasiri.**

Tarehe ya kuanza masomo kwa mwaka wa masomo 2019/2020 ni 14/10/2019.

**NB:**

- Maombi yote yatumwe Chuoni ndani ya muda uliopangwa
- Fomu za maombi ziambatanishwe na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay-in Slip) yenye kiasi cha Tshs. 10,000/= na ilipwe kwenye akaunti ya Chuo (**Akaunti Na. 01J1082316900, CRDB, CHUO CHA MADINI DODOMA).**
- Wanawake wanahamasishwa zaidi kutuma maombi
- Chuo hakitoi ufadhili kwa wanafunzi watakaochaguliwa katika kozi zote

Fomu za maombi zitumwe kwa: **Mkuu wa Chuo,**
**Chuo cha Madini Dodoma**
**S.L.P 1696,**
**Dodoma**

**Baruapepe: principal@mri.ac.tz**
**Simu: +255 26 296 3004**
,





**Picha na:**

i. Wizara ya Madini
ii. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Idara ya Habari - MAELEZO
iii. Chuo cha Madini Dodoma (MRI)
iv. Mgodi wa Buzwagi
v. Mgodi wa Mwadui (Williamson Diamond Mine/Petra Diamonds)
vi. Mgodi wa Geita (GGM)
vii. Mgodi wa North Mara/Acacia



JARIDA LA
**NCHI YETU**
TANZANIA

# WIZARA YA MADINI

**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**S. L. P 422,**
**40474 Dodoma.**

Simu: +255 26230051,
Nukushi: +255 26 2322282
Baruapepe: ps@madini.go.tz

Jarida hili la "**NCHI YETU**" ni toleo la kwanza maalum la Wizara ya Madini ambalo limechapishwa kueleza maendeleo na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kuwa mchango wa Sekta ya Madini katika uchumi wa nchi unaongezeka.

www.madini.go.tz